# Nipashe

Alhamisi Desemba 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581517

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital | epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




UKURASA 22

**GUARDIOLA: TUTABEBA TENA UBINGWA WA EPL**

# HALI TETE

• **Katesh**, Kilosa miili zaidi yaopolewa • **Mvua** yaangusha nyumba 51 Shinyanga • **Kote** ni vilio vya kaya zisizo na makazi... *Endelea ukurasa 2&4*



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Ibanza, Kata ya Mwamala wilayani Shinyanga wakiwa nyumbani kwa mmoja wa waathirika wa mvua ya mawe iliyonyesha usiku wa jana na kusababisha nyumba 51 kuanguka. **PICHA: MARCO MADUHU**



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Fredrick Shoo, akibariki kaburi la aliyekuwa Askofu mstaafu Dk. Erasto Kweka (89), baada ya kuzikwa kwenye lango kuu la Kanisa KKKT Usharika wa Uswaa, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MARY MOSHA**

" Mwaka 1995 nilipata fursa ya kufundisha programu maalum ya demokrasia na haki za binadamu, ambayo ilikuwa imeanzishwa na KKKT. Sasa wakati ninafanya programu hiyo, aliona kipaji changu cha siasa... **Tundu Lissu**





" Alikuwa kiongozi wa dini mwenye busara kubwa zaidi wakati huo. Kama kuna jambo halielewi serikalini, alikuwa akikuita na mimi aliniita mara nyingi na kuongea naye. **Frederick Sumaye**

# Sumaye: Kweka alituongoza tulipokwama kikazi serikalini

• **Lissu** amtaja ndiye alimnoa kisiasa... *Endelea ukurasa 3*


**UKURASA WA 3**
**Wastaafu** waidai UDSM mabilioni, yenyewe yakana

**UKURASA WA 17**
**Zanzibar** walia na utelekezaji watoto uliozidi

**UKURASA WA 19**
**Waangalizi** DRC: Wagombea acheni sentensi za ukabila


## Samia, Mbowe kutua msibani Katesh leo

UKURASA 2


**MICHEZO** **GAMONDI AONGEZA DOZI YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Hali tete Kilosa, Shinyanga, Katesh

## • Rais Samia, Mbowe kutua Hanang' leo




Baadhi ya askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) wakiondoa tope katika maeneo ya Mji Mdogo wa Katesh, wilayani Hanang', mkoani Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**

**Na Waandishi Wetu**

HALI ni tete! Ndicho unachoweza kusema kutokana na kinachoendelea katika wilaya za Hanang', Shinyanga na Kilosa.

Idadi ya vifo vilivyotokana na maporomoko ya tope toka mlima Hanang' huko Katesh, wilayani Hanang' mkoani Manyara vimeongezeka hadi 69 kufikia jana jioni, huku vifo vingine vya watu wawili vikiripotiwa jana wilayani Kilosa, mkoani Morogoro kutokana na mafuriko.

Wakati hali ikiwa hivyo Hanang' na Kilosa, wilayani Shinyanga mkoani Shinyanga nako hali ni tete. Nyumba 51 katika Kijiji cha Ibanza zimeanguka kutokana na mvua ya mawe iliyonyesha.

### YANAYOJIRI KATESH

Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson jana alitembea yaliyokotokea maafa katika Kata ya Katesh na kuwapa pole wananchi waliokumbwa na janga hilo.

Kiongozi huyo wa Bunge pia alikabidhi misaada ya kibinadamu kwa niaba ya wabunge na kampuni za simu zilizoungana na serikali zikitoa msaada wenye thamani ya Sh. milioni 240.

Dk. Tulia alisema wabunge wametoa kilo 3,000 za mchele, kilo 3,000 za unga, kilo 800 za maharagwe, viroba 30 vya sabuni na katoni 15 za mafuta ya kupikia.

Aliwaomba wananchi kuendelea kuwa wavumiluvu, akisisitiza kuwa wabunge wako pamoja nao na wanawapa pole.

"Ninaipongeza timu yote, wakiongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama, kwa kazi nzuri waliyofanya," alisema Spika Tulia.

Waziri Jenista, akigawa msaada kwa waathirika waliopewa hifadhi katika Shule ya Sekondari Katesh, alisema jumla yao ni 205.

Alisema kuwa katika kutoa huduma kwa wananchi waliopatwa na majanga, wamefanikiwa kuokoa watu wengi zaidi kulinganishwa na vifo. Majeruhi wote wamepatiwa mahitaji ikiwamo matibabu na chakula.

Vilevile, alisema wameishapokea mitambo 18 ya kusaidia kuondoa tope na kurekebisha miundombinu iliyoharibiwa. Alibainisha kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anayetarajiwa kutembelea Katesh leo, ameshaelekeza walioathirika wapatiwe chakula na dawa ndani ya siku 30.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana alasiri, alibainisha kuwa vifo vimeongezeka na kufikia 69 toka 65 vilivyoripotiwa hadi kufikia juzi alasiri. Kati ya vifo vinne vilivyoongezeka, viwili ni vya wanaume.

Matinyi pia alisema miili 68 imeshatambuliwa na ndugu zao na mwili mmoja ndio haujatambuliwa mpaka kufikia jana alasiri.

Kuhusu majeruhi, kiongozi huyo alisema 45 walikuwa wanaendelea na matibabu hospitalini huku waathirika 291 wakiwekwa kambini.

Meneja wa kampuni ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania Kanda ya Kaskazini, Andrew Temu, akiwakilisha umoja wa kampuni za mawasiliano ya simu nchini, alisema misaada waliyoitoa kwa ajili ya waathirika wa janga hilo, ina thamani ya Sh. milioni 240.

Temu alibainisha msaada wao umejumuisha mchele, unga wa ngano na unga wa mahindi, mablanketi, magodoro, sabuni na maji ya kunywa, vyote vikitolewa na Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel.

### SALAMU ZA TEC

Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) nalo limetoa misaada ya vitu mbalimbali kwa wananchi wa Katesh waliokumbwa na maafa yaliyosababishwa na mafuriko na maporomoko ya udongo.

Vitu vilivyotolewa na baraza hilo ni mablanketi, dawa za hospitalini, chakula na baadhi ya pembejeo za kilimo hasa mbegu kwa ajili ya kupandwa kwenye mashamba yaliyoathirika.

Rais wa TEC, Askofu Gervas Nyaisonga, alibainisha kutolewa msaada huo alipozungumza na waandishi wa habari jana jijini Mbeya. Alisema tayari vitu vilivyotolewa na baraza hilo vilikuwa vimeshaanza kusafirishwa kwenda mkoani Manyara.

Alisema baraza hilo limeshatia saini waraka maalum wa kukabidhi msaada huo kwa viongozi wa Mkoa wa Manyara ambao nao watakabidhi kwa wananchi waliopata madhara ya mafuriko hayo.

"Msaada huu si wa mwisho, tunaendelea kuwasiliana na washirika wetu pamoja na wahisani wa ndani na nje ili tuendelee kushirikiana kutoa misaada kwa sababu tunajua haya ni maafa makubwa," alisema Askofu Nyaisonga.

Alisema baraza hilo linatoa pole kwa wananchi wote wa Tanzania pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali kutokana na maafa hayo yaliyotokea wilayani Hanang'.

Alisema taarifa walizokuwa wamezipata mpaka kufikia jana ni kwamba zaidi ya watu 5,000 walikuwa wameathiriwa na mafuriko hayo huku zaidi ya watu 60 wakipoteza maisha na wengine 116 walikuwa wamejeruhiwa ambao.

Alisema zaidi ya kaya 1,150 ziliathirika kwenye mafuriko hayo na hivyo wakazi wa eneo hilo wanahitaji msaada wa hali na mali ili kuokoa maisha yao pamoja na vitu vingine.

### MVUA YA MAWE

Wakati TEC ikichukua hatua hizo, mvua ya mawe iliyonyesha katika Kijiji cha Ibanza, Kata ya Mwamala wilayani Shinyanga, imesababisha nyumba 51 kuanguka na kuathiri mashamba ya mahindi na mifugo, huku baadhi ya wananchi wakinusurika kifo kwa kuangukiwa na nyumba hizo.

Imeelezwa kuwa nyumba hizo zilianza kuanguka saa tisa usiku wa kuamkia jana wakati wananchi wakiwa wamelala kwenye nyumba zao.

Mmoja wa wanakijiji huko Ibanza, Jilala Dutu, aliiambia Nipashe jana kuwa wakati mvua hiyo inanyesha majira hayo ya usiku, walishaghaa kuona mabati yakibebwa na upepo na kisha maboma kuanguka.

"Ukuta uliangukia ndani, tofali likamponda mtoto kichwani, na mama mkwe ambaye amevunjika mguu. Kwa sasa yuko Hospitali ya Rufani (ya Mkoa wa Shinyanga) akipatiwa matibabu," alisema Dutu.

Mwanakijiji mwingine, Nkuba Jigadi alisema nyumba yake imeangushwa na mvua hiyo ilipoharibu pia shamba lake la mahindi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliyewatembelea wanakijiji hao, alitoa pole kwao na kueleza kuwa kwa tathmini ya awali, nyumba 51 zimeanguka na kuharibu mashamba ya mahindi ekari 10.

Alisema serikali iko pamoja na waathirika hao. Wananchi ambao wameumia, serikali itagharamia matibabu yao na itawapatia mbegu za mahindi bila malipo.

### VIFO KILOSA

Wakati hali ikiwa hivyo wilayani Shinyanga, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, amesema kaya 327 zimeathiriwa na mafuriko katika kata za Mvumi na Rudewa.

Alisema mpaka sasa jumla ya vifo vitatu vimetokea mafuriko hayo. Watu wawili walifariki dunia jana majira ya mchana wakiwa katika harakati za kujiokoa.

"Tumekuwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima. Tumewatembelea na kutoa pole kwa wahanga (waathirika) wa mafuriko. Hadi mchana wa leo (jana), vifo vingine viwili vimetokea ambao ni Charles Mnange (19), mkazi wa Rudewa Batini, Kijiji cha Makuruge, aliyeteleza na kutumbukia katika Bonde la Mto Wami akiwa katika harakati za kujiokoa.

"Mwingine ni Nelson Yona (18), mkazi wa Ifuga Mbigiri aliyefariki (dunia) baada ya kuzama kwenye kina kirefu cha maji ya Mto Gekuru na kusababisha iddai ya vifo kufikia vitatu kutokana na mafuriko hayo," alifafanua.

Shaka alisema serikali inaendelea kufanya tathmini ya mafuriko huku wakiendelea kutoa huduma za kibinadamu kwa waathirika hao.

Miezi mitatu iliyopita, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilizitaka mamlaka husika za serikali na wananchi kuchukua tahadhari kutokana na uwezekano wa nchi kupata mvua kubwa za El-Nino mwaka huu.

### MBOWE HANANG

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, leo anatarajiwa kutembelea Hanang' kwa ajili ya kuwafariji waathirika na kutoa pole na faraja kwa familia zilizopoteza wapendwa wao.

Taarifa iliyotolewa jana na uongozi wa Kanda ya Kaskazini wa CHADEMA, ilibainisha kuwa Mbowe ataongozana na Mwenyekiti wa Kanda hiyo, Godbless Lema na viongozi wa chama hicho wa wilaya na mkoa wa Manyara.

Akiwa Hanang', Mbowe atawatembelea waathirika walioko Hospitali ya Manyara na Wilaya ya Hanang' na walioko katika makambi na familia, kisha kuzuru Kijiji cha Gendabi kujionea hali halisi ya madhara ya mafuriko hayo na kuona juhudi za uokoaji zinazoendelea na kukutana na wananchi ili kutoa pole na faraja.

"Uongozi wa Kanda Kaskazini CHADEMA utaendelea kuwaomba Watanzania wote hasa waliopo Kanda ya Kaskazini kujitokeza kutoa nguvu kazi pamoja na misaada ya utu na faraja kwa familia zilizopatwa na janga hilo," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

***Imeandaliwa na Jaliwason Jasson (MANYARA), Nebart Msokwa (MBEYA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Beatrice Shayo (MOROGORO) na Romana Mallya (DAR)**

## HABARI KITAIFA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza kwenye Kongamano la Kimataifa la Wanawake katika Biashara Huru Afrika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sumaye: Askofu Kweka alituongoza tulipokwama kikazi serikalini

**Na Waandishi Wetu,** HAI

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye, ametoboa siri Askofu Mstaafu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Erasto Kweka, alivyokuwa akiwaita viongozi wa serikali na kuwashauri yalipokuwa yakitokea mambo magumu ambayo Watanzania walitaka majibu.

Sumaye alidokeza jana kuhusu busara alizokuwa nazo Askofu Dk. Kweka wakati wa uhai wake, wakati wa ibada ya maziko ya kiongozi huyo mkongwe wa kiroho iliyofanyika katika viwanja vya Usharika wa Uswaa, Hai mkoani Kilimanjaro.

Ibada hiyo ya maziko hayo iliongozwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Frederick Shoo, akisaidiwa na Mkuu wa KKKT Mteule, Askofu Dk. Alex Malasusa, na Askofu Mstaafu wa KKKT Dayosisi ya Iringa, Prof. Owdenburg Mdegella huku maaskofu 29 wa kanisa hilo wakihudhuria.

Askofu Dk. Kweka, alifariki dunia Novemba 25, mwaka huu, katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam, wakati akipatiwa matibabu.

"Namkumbuka sana Askofu Dk. Kweka kama mtu wa kazi na mwenye upendo wa ajabu, hasa katika kushauri mambo mbalimbali. Alikuwa kiongozi wa dini mwenye busara kubwa zaidi wakati huo. Kama kuna jambo halielewi serikalini, alikuwa akikuita na mimi aliniita mara nyingi na kuongea naye ili kupata ufafanuzi.

"Kama hajakuelewa, utamwelewesha. Ikiwa hajaelewa atakushauri na kutaka mkatafakari upya. Kwetu alikuwa mtu wa karibu sana, anayeshauri na anayependa mabadiliko chanya. Kwa kweli atabaki kuishi kwenye mioyo yetu." alisema Sumaye.

### LISSU AFUNGUKA

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akitoa salamu za chama hicho, alisema Askofu Dk. Kweka, ndiye aliyekitambua kipaji chake cha siasa na kumshauri agombee kiti cha ubunge akiwa na umri wa miaka 27.

"Mwaka 1995 nilipata fursa ya kufundisha programu maalumu ya demokrasia na haki za binadamu, ambayo ilikuwa imeanzishwa na KKKT. Sasa wakati nafanya programu hiyo, aliona kipaji changu cha siasa na kunisisitiza nigombee nikiwa na miaka 27, ingawa niligombea na kushindwa na sikukata tamaa.

"Askofu Dk. Kweka, alikuwa baba mwenye maono na mitazamo inayoleta tija kwa jamii. Alikuwa mshauri na mfuatiliaji wa mambo, hasa anapoliona likiwa na tija kwa jamii. Kama tunataka kwenda kuwa naye, tuige matendo yake," alisema.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu Prof. Mdegella alisema Dk. Kweka atakumbukwa kwa uaminifu wake katika kusimamia mambo mengi ikiwamo miradi ya maendeleo.

Katika maziko hayo, Rais Samia Suluhu Hassan aliwakilishwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa. Viongozi wengine ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, na Mbunge wa zamani wa Arusha, Godbless Lema.

Askofu Dk. Kweka atakumbukwa kwa kuasisi KKKT kuwa wachungaji wa kike ndani ya kanisa wakiwamo wanaotumika katika Dayosisi mbalimbali na wengine taasisi za elimu ambao ni madaktari wa falsafa na maprofesa.

Pia Dk. Kweka ndiye aliyeasisi kuanzishwa Shirika la Watawa wa Usharika wa Neema, kitu ambacho hakikuwahi kudhaniwa ndani ya kanisa.

Dk. Erasto Kweka aliyehudumu kama Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini kwa miaka 28, baada ya kufariki dunia aliyekuwa Mkuu wa Kwanza wa KKKT nchini, Dk. Stefano Moshi, atakumbukwa pia kwa alama nyingine isiyofutika ya kuanzishwa Chuo Kikuu Kushiriki cha Sayansi ya Tiba cha KCMCo.

Aidha, wakati wakati akihudumu kama Askofu, ndiye aliyeiongoza KKKT kuridhia kupandisha hadhi Hospitali ya KCMC kuwa Hospitali ya Rufani.

Pia atakumbukwa kama mbeba maono na mwanzilishi wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha ELCT-ND 1994, ambacho kinashika nafasi ya tatu kwa ukubwa wa mitaji nchini, kikiwa na zaidi ya Sh. bilioni 10.

Askofu Dk. Kweka alibarikiwa kuwa Mchungaji mwaka 1965 kabla ya kuwa Msaidizi wa Askofu Dk. Moshi ambaye alikuwa Mkuu wa kwanza wa Dayosisi ya Kaskazini.

Alichaguliwa kuwa Askofu wa pili wa Dayosisi hiyo mwaka 1977 akipokea kijiti hicho kwa Askofu Dk. Stefano Moshi na kuhudumu katika wadhifa huo hadi mwaka 2004, alipochaguliwa Askofu Dk. Martin Shao, kumrithi.

***• Imeandikwa na Mary Mosha na Godfrey Mushi***

# Wastaafu UDSM wasotea madai ya bilioni 300/- kwa miaka 40

**Na Enock Charles**

ZAIDI ya wastaafu 3,500 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wameiomba serikali kuingilia kati ili walipwe stahiki mbalimbali wanazodai kwa zaidi ya miaka 40.

Stahiki hizo ni mafao, nauli, mabati na saruji kutokana na utumishi wao katika chuo hicho ambazo wamedai hawajalipwa mpaka sasa licha ya kuhangaikia kwa muda mrefu.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita, baadhi ya wastaafu hao walisema wamehangaikia mafao hayo kwa zaidi ya miaka 40 bila mafanikio, hivyo kuiomba serikali kuwasaidia.

Katibu wa Kamati ya Wazee Wastaafu wa kilichokuwa Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Evarist Majaliwa, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema wanadai zaidi ya Sh. bilioni 300.

"Sisi tunachohitaji ni kulipwa madai yetu ambayo kwa kweli ni ya muda mrefu. tumeshahangaika sana tangu enzi ya Mwalimu (Julius) Nyerere mpaka sasa.

"Tumeanza harakati hizi za kupambania madai yetu tangu mwaka 1978 Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipovunjika na wengine wenzetu wameshafariki dunia bila kuonja hata chembe ya mafao licha ya kulitumikia taifa kwa uzalendo mkubwa," alisema.

Wazee hao ambao wengi wao wamedai kustaafu tangu mwaka 1977, walisema wamewasilisha madai yao katika chuo hicho na ofisi mbalimbali za serikali, ikiwamo Wizara ya Fedha lakini wameambulia patupu.

Pia, alisema katika wastaafu hao, kuna kundi lingine la waliostaafu mwaka 1996 ambao nao wanadai kutokulipwa madai yao yanayofikia zaidi ya Sh. bilioni 331 na vitu vingine, vikiwamo mabati na saruji waliyoahidiwa kulipwa, lakini hawakupewa huku wakionyesha nyaraka mbalimbali za madai yao katika ofisi mbalimbali.

### CHUO CHAJIBU

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa UDSM, Asha Hayeshi, licha ya kukiri kutambua madai hayo, alisema si madai ya kweli kwa kuwa hayapo popote katika kumbukumbu za chuo na pia wazee hao hawajathibitisha kukidai chuo hicho licha ya kwenda mpaka mahakamani na katika Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupeleka madai yao.

"Hao wa mwaka 1977 hawajaja kwa muda mrefu hapa lakini hao wa mwaka 1996 walikuja mara ya mwisho ni wiki mbili tu zilizopita, hakuna mwenye nia mbaya ya kukataa kuwalipa kwa sababu wengine wakati huo hatukuwepo, isipokuwa wameshindwa kuthibitisha madai yao licha ya kwenda mpaka mahakamani," alisema Hayeshi.

"Barua za Hazina zinathibitisha kuwa jumuiya ilipovunjika watu wote walilipwa na kwamba hawana madai yoyote, kuhusu hao wa mwaka 1996 tumeshakaa nao vikao mara kadhaa kwa ajili ya kuwasikiliza mara zote kutaka kujua madai yao hasa ni nini kwa sababu walishalipwa," aliongeza.





Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana na Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja (katikati), akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba (kushoto) na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Paul Kijazi, alipotembelea ofisi za PSSSF jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yakabidhi msaada kwa waathirika wa maporomoko

**Na Mwandishi wetu**

WAATHIRIKA wa mafuriko yaliyotokea wilayani Hanang, mkoani Manyara waliopoteza ndugu zao, makazi na mali, wamepatiwa msaada ya kibinadamu na Benki ya NMB ikiwamo magodoro na vyakula ili wapate mahitaji muhimu baada ya kupata janga hilo la mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia Jumapili iliyopita na kusababisha mafuriko ya tope zito katika eneo hilo.

Mchango wa benki hiyo ulikabidhiwa jana na Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Kaskazini, Baraka Ladislaus, katika ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Hanang' na kupokelewa na Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara, Asia Halamga.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Ladislaus alisema wanaungana na serikali katika kipindi hiki ambacho wananchi wengi wamepoteza maisha, kuharibika kwa miundombinu na kuacha mamia ya wananchi wakiwa hawana makazi.

Alitaja misaada hiyo kuwa ni magodoro 100, mablanketi 40, maji, mafuta na vyakula mbalimbali ikiwamo mchele na maharage.

"Tunawapa pole sana na tunajua pametokea msiba mzito na madhara yamepelekea kuharibika kwa miundombinu, mali za watu wetu na kusababisha vifo.

"Tumekuja kuwapa pole wananchi wa Manyara na benki itaendelea kushirikiana nao kutoa huduma mbalimbali za kifedha pale itakapohitajika.

"Tunatambua pia kuna wengine wana bima na sisi kama benki, najua wale wanaopata huduma kwetu tutaendelea kurudisha hali hiyo kuhakikisha wanapata malipo yao ya bima kwa wakati," alisema.

Akipokea kwa niaba ya mkoa, Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha vijana wa Mkoa wa Manyara, Asia Halamga, amesema wanashukuru benki hiyo na kuomba wadau wengine kujitolea kusaidia waathirika wa janga hilo.

"Tunawashukuru sana NMB kwa msaada huu, mmetukimbilia wana Manyara. Tatizo ni kubwa tunahitaji msaada kwa wananchi wetu, tunaomba wadau wenye nafasi ya kutoa msaada mtuunge mkono," alisema.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | MADALE KIKDS PALACE | KWENYE HATI NAMBA DSMT1001536 | CRUCIAL INVESTMENT LIMITED | MADALE-KINONDONI | 21/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | SHADRACK AMONI SANGA | NYUMBA | NELSON WILFRED SANFA | KIMARA GOLANI | 21/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | NYUMBA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | MWANDEGE-MKURANGA | 22/12/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ANNA DEOGRATIUS MSEMA | NYUMBA | DEOGRASIUS PETER MSEMA | SINZA | 27/12/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0785242219/0719351040
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.


# Walia serikali kuchelewesha maboresho ya Sheria ya Ndoa

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI) kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WilDAF), wameiomba serikali kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Kwa mujibu wa wadau hao, sheria hiyo imewapa nguvu wanaume na familia kutumia upungufu uliopo kama fursa ya kuozesha watoto.

Mratibu wa Kitaifa wa WilDAF, Anna Kulaya, alisema juzi jijini Dar es Salaam kuwa sheria hiyo pia imesababisha dosari kwa sheria zingine kama vile Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Anna alisema kuwa katika kipindi hiki cha kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia, kuna haja ya serikali kuchukua maoni yanayotolewa na wadau na kuyafanyia kazi.

Alisema ucheleweshaji marekebisho hayo ya kisheria, umeendelea kusababisha watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo na kukumbana na ukatili wa kijinsia kwa kushindwa kuhimili mikiki ya ndoa.

"Tunatambua kwamba serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria iko kwenye mchakato wa kukusanya maoni ya wadau juu ya umri wa mtoto wa kike kuolewa.

"Hata hivyo, mchakato huu umechukua muda mrefu kufuatia uamuzi ya kesi ya Rebeca Gyumi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na rufani ya madai namba 204 ya mwaka 2017 katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania jijini Dar es Salaam.

"Katika hukumu yake iliyotolewa Oktoba 15 mwaka 2019, mahakama ilikiona kifungu cha 13 na cha 17 cha Sheria ya Ndoa Sura 29 kuwa kinyume cha Katiba na kuiamuru serikali kufanya marekebisho ya sheria hiyo ya ndoa ndani ya mwaka mmoja, lakini mpaka sasa sheria hiyo haijafanyiwa mabadiliko," alilalama.

**Katika hukumu yake iliyotolewa Oktoba 15 mwaka 2019, mahakama ilikiona kifungu cha 13 na cha 17 cha Sheria ya Ndoa Sura 29 kuwa kinyume cha Katiba na kuiamuru serikali kufanya marekebisho ya sheria hiyo ya ndoa ndani ya mwaka mmoja, lakini mpaka sasa sheria hiyo haijafanyiwa mabadiliko.**

Alisema ni vyema serikali ikaharakisha mchakato wa maboresho ili wasichana na watoto wa kike walindwe kisheria.

Hivi karibuni akifungua kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema serikali kupitia wizara yake pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria, inafanya mchakato kuhakikisha sheria zote zinazomhusu mtoto zinasomana.

Kampeni hiyo ilizinduliwa Novemba 25 mwaka huu ikiwa na kaulimbiu ya 'Wekeza Kuzuia Ukatili wa Kijinsia".

## SIKU YA USAFIRI WA ANGA DUNIANI

TCAA CONSUMER CONSULTATIVE COUNCIL

# MATUMIZI YA UBUNIFU NA TEKNOLOJIA KATIKA KUTATUA CHANGAMOTO MBALIMBALI ZA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA



***Bw. Innocent Kyara, Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA CCC)***

Kila tarehe 07 mwezi Disemba, wadau wa usafiri wa anga huadhimisha siku ya usafiri wa anga duniani. Siku hii inatambuliwa na Umoja wa Mataifa (UN) kwa lengo la kuongeza uwelewa juu ya umuhimu wa sekta ya usafiri wa anga katika kuchochea maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii miongoni mwa nchi wanachama.

Kauli mbiu ya mwaka huu katika kuadhimisha Siku ya Usafiri wa Anga Duniani ni "Matumizi ya ubunifu katika maendeleo ya usafiri wa anga duniani". Kauli Mbiu hii imetumika kwa miaka mitano mfululizo, tangu mwaka 2019 kufuatia maazimio yalitotolewa Baraza la Uongozi la Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO).

Katika kuadhimisha siku hii na kwa kuzingatia kauli mbiu husika, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA CCC) linaangazia kwa namna gani matumizi ya ubunifu na teknolojia yanavyoweza kutumika kutatua baadhi ya changamoto wanazokutana nazo watumiaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

Ikumbukwe, TCAA CCC ndiyo chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 kwa lengo la kumlinda na kumtetea mtumiaji wa huduma za usafiri wa anga. Hivyo, taasis hii inao wajibu wa kuwasemea watumiaji na kushauri wadau wa usafiri wa anga juu ya hatua za kuchukua kukabiliana na masuala mbalimbali ambayo yanamuathiri mtumiaji wa huduma za usafiri wa anga kwa maendeleo endelevu ya sekta ya usafiri wa anga nchini.

Mwezi Mei mwaka huu 2023, kulifanyika ukaguzi wa masuala ya ulinzi katika viwanja vya ndege chini ya program maalum ya ICAO (Universal Security Audit Program Continuous Monitoring Approach) na Nchi yetu kufanikiwa kupata alama 87%.

Alama hizi zimetuwezesha Tanzania kuvuka wastani wa asilimia 80 ambao ndio malengo ya ICAO, kwa nchi zote kufikia wastani huo ifikapo 2023. Aidha, miongoni mwa maeneo ambayo yalitupunguzia alama na kusababisha nchi yetu kushindwa kupata asilimia 100 ni katika maeneo ya uwezeshaji abiria (security aspect of passenger facilitation) pamoja na maeneo ya ulinzi wa abiria na mizigo yao (Passenger and Baggage Security). Tayari mpango wa marekebisho wa mapungufu yaliyoainishwa katika taarifa ya ukaguzi huo (Corrective Action Plan) umeshaandaliwa na kuanza kutekelezwa ikiwemo uanzishwaji wa mchakato wa usimbikaji mfumo wa utumaji taarifa za watumiaji wa huduma za usafiri wa anga (Advanced Passenger Information (API) and Passenger Name Record).

Mifumo hii itawezesha kubadilishana taarifa za abiria wa ndege baina Idara ya Uhamiaji nchini na mataifa mbalimbali kwa lengo la kuzuia wahalifu kuingia nchini kwetu kwa kufanya utambuzi wa wahalifu hao mapema kabla hawajaingia nchini. Ikumbukwe ulinzi wa taarifa hizi binafsi za watumiaji umehakikishwa kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (The Personal Data Protection Act, Cap 44) ikisomwa pamoja na Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi, 2023.

Mapema mwezi Novemba, 2023, Baraza la Umoja wa Ulaya (linalohusisha jumla ya nchi 27) lilifikia uamuzi wa kuanza kutoa visa katika eneo la Schengen kwa njia ya kidigitali.

Kufuatia maamuzi haya, matumizi ya kibandiko cha VISA (VISA Sticker) yataachwa na badala yake itatumika teknolojia ya kriptografia (Cryptography). Matumizi ya teknolojia hii yanatoa ulinzi na siri za taarifa za mtumiaji zinazopatikana katika vibandiko vya visa. Aidha, teknolojia hii inawezesha mashirikiano baina ya taasisi zinazohusika na uhamiaji (cross-border collaboration).

Katika hatua nyingine, imekua ni lazima tangu June 2008 kwa wanachama wa Umoja wa Mashirika ya Ndege Duniani (IATA) kutoa tiketi mtandao (e-ticket) ambapo wakati wa kuthibitisha safari (check-in), abiria amekua akihitajika kuwasilisha kitambulisho chake pekee.

Kisha, karatasi huchapishwa na kupatiwa abiria kama kibali cha kumruhusu kuingia ndani ya ndege (boarding pass). Hatua hii huenda sambamba na kuchapisha karatasi nyingine (baggage check tag) inayofungwa kwenye mzigo wake unaoingizwa ndani ya ndege, kwa ajili ya utambulisho.

Gharama za kununua na kuchapisha karatasi hizi zimekuwa ni kubwa na zipo taarifa kwa baadhi ya mashirika ya ndege yanayofanya safari zake nchini kuwasilisha mapendekezo kwa Serikali kuondoa baadhi ya kodi katika karatasi hizi kama njia ya kuchochea ukuaji wa sekta ya usafiri wa anga nchini.

Kwa kutambua changamoto hii, baadhi ya mashirika ya ndege duniani yameanza kutumia mfumo wa kielekroniki (electronic boarding pass) ambapo mara baada ya abiria kuthibitisha safari yake, hutumiwa ruhusa yake ya kuingia katika ndege (boarding pass) kwenye barua pepe hivyo kuondokana na takwa la kuchapisha karatasi hiyo. Aidha, baadhi ya viwanja vya ndege vimekwenda mbali na kuweka teknolojia/miundombinu inayofanya utambuzi wa abiria ambao wamethibitisha safari zao (facial recognition) bila ya kuonesha vibali husika (boarding pass) hivyo kuokoa muda na kurahisisha abiria kusonga kwa haraka.

Ikumbukwe, mlipuko wa homa ya Uviko 19 (Covid19), ambapo mapambano dhidi ya kusambaa kwa ugonjwa huu yalihitaji kuepuka misongamano na mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtoa huduma na abiria, ulichochea uvumbuzi na kuongeza matumizi ya teknolojia hii.

Hivyo ni rai yetu kwa wadau wa usafiri wa anga nchini kufikiria kuanza kutumia teknolojia hii ya utambuzi wa sura (facial recognition) na utoaji wa hati za kielektroniki (electronic boarding pass) kama njia ya kudumu ya kupambana na magonjwa ya mlipuko yanayosambazwa kwa njia ya hewa katika viwanja vya ndege nchini.

Aidha, yako baadhi ya mashirika duniani ambayo yanatoa karatasi za utambuzi wa mizigo ya abiria (baggage check tag) zenye kisimbuzi cha kusaidia ufuatiliaji wa mzigo ulipo (tracking device) hivyo kusaidia katika kutafuta mabegi ya abiria yaliyopotea (lost baggages).

Teknolojia hii inasaidia upatikanaji wa mizigo ya abiria kwa haraka na kupunguza usumbufu kwa abiria husika kwani mizigo yake huweza kupatikana ndani ya muda mfupi. Hivyo, iko fursa kwa mashirika yetu ya ndege nchini kuanza kutumia ubunifu na teknolojia hii.

Kasi ya ukuaji wa teknolojia duniani inaenda sambamba na uwepo wa mtandao wa uhakika unaopatikana wakati wowote na sehemu yoyote ili kuwezesha watumiaji kuendelea na shughuli zao za kiuchumi bila mkwamo wowote.

Mwezi Oktoba 2023, Shirika la Ndege la Qatar lilitangaza kuingia mkataba na Kampuni ya Space X Starlink inayomilikiwa na tajiri mkubwa duniani Elon Musk ili kuwapatia wateja wake huduma ya mtandao wenye kasi kubwa wanapokuwa hewani. Kupitia huduma za Starlink wateja wa Shirika hilo la ndege wanapata kasi ya mtandao inayoweza kufikia hadi Megabits 350 kwa sekunde kulinganisha na kasi ya megabit 10 kwa sekunde iliyokuwa inapatikana hapo awali.



***Chumba cha Kuongoza Ndege katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA)***

Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) katika baadhi ya ndege zake hutoa hadi 20 MB bure endapo mtumiaji atahitaji huduma ya mtandao wakati wa safari. Hatua hii ni mwanzo mzuri kuelekea kuchochea ukuaji wa uchumi wa kidijitali nchini.

Aidha, Taasisi mbalimbali za Serikali zimeendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto wanazokutana nazo wananchi kwa kutumia teknolojia mbalimbali zitumiwazo katika usafiri wa anga.

Mathalani, katika kukabiliana na changamoto ya matumizi ya vinyunyizi vya kubeba mgongoni (matabi) kwa wakulima wenye mashamba makubwa, Serikali kupitia Bodi ya Pamba imenunua Ndege 20 zisizokuwa na rubani (drone) kwa ajili ya kunyunyuzia dawa. Ndege hizo zina uwezo wa kupuliza ekari 15 hadi 20 kwa saa moja, jambo ambalo linampunguzia adha mkulima.

Uvumbuzi wa madini ya kimkakati katika maeneo mbalimbali nchini umeleta fursa mpya katika sekta ya anga na kwa namna ya kipekee sekta ya madini kuwa na mchango wa moja kwa moja katika sekta ya anga.

Mathalani, madini ya graphite hutumika katika utengenezaji wa mabawa ya ndege, wakati madini mengine aina ya Nickel nayo hutumika katika kutengeneza engine za ndege.

Tayari nchi yetu imeshuhudia kutengenezwa kwa ndege aina ya Skyleader 600 iliyotengenezwa mkoani Morogoro na wataalamu wazawa kwa kushirikiana na Kampuni ya Airplanes Africa Limited (AAL) kutoka Jamhuri ya Czech.

Ndege hiyo uwezo wa kubeba rubani na abiria mmoja na kutumia wastani wa lita 15 za petroli kwa saa.

Ndege hiyo ilioneshwa kwa mara ya kwanza katika Maonesho ya Kimataifa ya Wazalishaji wa bidhaa za Viwandani Tanzania (Tanzania International Manufacturers Expo, 2023) yanayoratibiwa na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade)

Kwa upande wa matumizi ya teknolojia katika kuimarisha usalama wa usafiri wa anga, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) inaendelea na mradi wa usimbikaji vifaa vya kisasa vya mawasiliano ya radio (Very High Frequency (VHF) Radio Communication Systems) katika Viwanja vya ndege kumi na tano (15) nchini. Mradi huo tayari umefikia asilimia 65 ya utekelezaji wake.

VHF hutumika kwa kiasi kikubwa katika mawasiliano ya ndege na vituo vya ardhini, pamoja na mawasiliano kati ya ndege zinazokaribiana hewani.

Mawasiliano ya VHF hutoa mawasiliano ya sauti kati ya ndege na vituo vya udhibiti wa trafiki wa anga (ATC), vituo vya kudhibiti viwanja vya ndege (GND), na vituo vya kudhibiti njia za kuondoka na kutua (TWR).

Hivyo, mfumo wa VHF ni muhimu katika kudhibiti usalama wa anga na kuhakikisha mawasiliano sahihi kati ya ndege na watoa huduma wa anga.

Uvumbuzi na teknolojia umekuwa na matokeo chanya katika sekta ya anga kwa kuleta mabadiliko makubwa ambayo yameongeza usalama, ufanisi, na uzoefu wa abiria kwa ujumla. Matumizi ya ubunifu na teknolojia yametoa suluhisho kwa changamoto mbalimbali zinazowakabili watumiaji wa huduma za usafiri wa anga.

Kupitia teknolojia, uzoefu wa abiria umeimarishwa kwa kuwa na huduma za mtandao, burudani na mifumo ya kisasa ya usafiri. Katika suala la usalama na ufuatiliaji wa ndege, mifumo ya kiteknolojia inatoa ufumbuzi wa kuaminika na wa hali ya juu, huku ikipunguza hatari na kuboresha usimamizi wa safari za anga.

Matumizi ya takwimu na uchambuzi wa taarifa yanasaidia katika kupunguza muda wa kutua na kupaa, kuongeza ufanisi wa safari, na kuboresha utabiri wa hali ya hewa katika anga.

Aidha, juhudi zinazofanywa kuboresha ufanisi wa nishati na kutafuta njia mbadala za nishati zinachangia kufanya usafiri wa anga kuwa endelevu zaidi na kupunguza athari za mazingira.

Kwa ujumla, ubunifu na teknolojia unaendelea kuwa kiungo muhimu kwenye maendeleo ya sekta ya usafiri wa anga.Tafiti mbalimbali zinazoendelea kufanyika zinatarajiwa kufungua njia kwa enzi mpya ya mafanikio katika anga na kuashiria siku zijazo zenye uzoefu bora zaidi, safari salama, na huduma zenye ufanisi kwa watumiaji wa huduma za usafiri wa anga.

Mwandishi wa Makala hii ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Anga Tanzania (TCAA CCC), taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 yenye wajibu wa kumwakilisha, kumlinda na kumtetea mtumiaji wa huduma za usafiri wa anga kupitia progam mbalimbali za uwezeshaji ili waweze kufaham haki na wajibu wao pindi watumiapo usafiri wa anga.

Watumiaji wa huduma za usafiri wa anga na umma kwa ujumla wanaweza kuwasiliana na Baraza kwa elimu na ufafanuzi zaidi wa masuala mbalimbali kuhusu usafiri wa anga kupitia mitandao yetu ya kijamii ya Instagram Youtube na Mtandao X (@tcaa_ccc) au kupiga simu ya bure nambari 0800 110 190 au kupitia anuani iliyoainishwa hapa chini;

**Katibu Mtendaji,**
**Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (T CAA CCC)**
**Majengo ya TBA Na. L1, Kiwanja Na. 6/2,**
**Mtaa wa Kilimani, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,**
**S. L. P 12242,**
**14110 DAR ES SALAAM**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ulinzi bidhaa za ndani sawa lakini zinatosheleza mahitaji?

**KWA** miaka kadhaa, viongozi wengi wa serikali hasa wanaosimamia sekta za biashara na uwekezaji wamekuwa wakizungumzia suala la kulindwa kwa wazalishaji wa ndani dhidi ya bidhaa zinazotoka nje. Suala hili pia limewahi kuzungumzwa mara kadhaa hata katika vikao vya bunge, huku wabunge wakisisitiza wazalishaji wa ndani walindwe na kuhimiza bidhaa kutoka nje zitozwe kodi na ushuru mkubwa.

Mbali na mawaziri hao, miaka kadhaa iliyopita, wazalishaji wa saruji, kwa maana ya viwanda vya ndani, walifanya mkutano uliowajumuisha viongozi wa Wizara za Viwanda na Biashara, wadhibiti ubora na viwango; na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakieleza magumu wanayopitia katika biashara zao huku kilio kikubwa kikiwa kodi kubwa lakini bei ya bidhaa zao zinalingana na zile za kutoka nje. Kwa mantiki hiyo, waliweka wazi kwamba katika hilo hakuna usawa katika biashara.

Safari hii tena, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amerejea na kusema kuna haja ya kuwalinda wawekezaji wa ndani dhidi ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Prof. Mkumbo amekwenda mbali zaidi akisema itungwe sheria itakayokuwa ya mizani sawa.

Prof. Mkumbo alizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kwanza cha kuunganisha magari madogo nchini kinachotarajiwa kuwekeza zaidi Sh. bilioni 10. Uwekezaji huo unafanyika zikiwa siku 25 tu tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipofanya ziara nchini India. Kuanzishwa kwa kiwanda hicho ni ushirikiano kati ya kampuni ya GF Automobile na Mahindra kutoka India.

Ni dhahiri kwamba uwekezaji huo utasaidia kuongeza wigo wa ajira kwa vijana wa Kitanzania ambao kwa miaka mingi wamekosa fursa hiyo lakini pia utasaidia kupatikana kwa magari nchini ambayo kwa namna fulani yatakuwa na bei ya chini kulinganisha na yale anayoagizwa moja kwa moja kutoka nje ya nchi.

Kauli ya Prof. Mkumbo ni nzuri na ilipaswa kuwa imeshaanza kufanyiwa kazi miaka mingi iliyopita kwa sababu Tanzania imepita katika hatua mbalimbali za kimaendeleo tangu Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 na baadaye Azimio la Arusha mwaka 1967.

Ili kupata majawabu ya hoja hiyo, kuna maswali kadhaa ya kujiuliza. Mosi, nini Tanzania imefanya tangu wakati huo kwa maana ya kuwa na bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vya ndani na hatimaye kutosheleza soko la ndani na kuuza ziada nje? Pili, bidhaa za ndani hata kama zinazalishwa kwa kiwango kidogo, zimelindwa vipi katika soko la ndani dhidi ya zile zinazoingizwa kutoka nje?

Ni vigumu kulinda bidhaa za ndani kama uwezo wa uzalishaji wa ndani ni mdogo. Ni wazi kwamba viwanda vya ndani vilivyopo hazina uwezo wa kutosheleza soko la ndni hivyo ni lazima kuwapo na uagizaji kutoka nje ili kuziba pengo la bidhaa lililopo.

Jambo la msingi linalopaswa kufanywa ni kujenga uwezo wa ndani ili kufikia hatua ya kulinda bidhaa zetu kabla ya kuanza kuweka vizuizi kwa sababu uzalishaji wa ndani haufiki hata robo ya mahitaji stahiki.

Nchi kama Malaysia, Singapore na Korea Kusini, maarufu kama Asian Tigers, zilifikia hatua hiyo baada ya uzalishaji wa ndani kuwa mkubwa kutosheleza soko la ndani. Iweje leo kuwe na wazo la kutungwa sheria ya kulindwa kwa bidhaa za ndani ilhali hata viberiti, chumvi, mafuta ya kula, vinywaji kama juisi, pombe kali na bia vinaagizwa nje?

Mafuta ya kula kwa mfano, zaidi ya Sh. bilioni 500 zinatumika kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje kwa maana kwamba uzalishaji wa ndani ni mdogo. Ni vyema kabla ya kufikia hatua hiyo, nguvu zaidi ikaelekezwa katika kuimarisdha uzalishaji wa ndani wa bidhaa anuai na ni vizuri matamko ya kisiasa yakaepukwa katika masuala nyeti kama haya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Elimu ya makuzi kwa vijana muhimu, ila kuifanikisha ni mtihani mwingine

**ELIMU** ya makuzi kwa vijana, hususan waliopo vyuo vikuu na vya kati, ni muhimu, ili kuwaweka kwenye usalama ikizingatiwa wanaojiunga na elimu hiyo wana umri mdogo.

Tangu serikali ianzishe mfumo wa wanaohitimu kidato cha nne kwenda moja kwa moja vyuoni, kumeleta athari chanya na hasi, huku baadhi yao kutokana umri mdogo kushindwa kutimiza malengo yao.

Hivi sasa si kitu cha ajabu kukuta mhitimu wa shahada ana umri usiozidi miaka 23, tofauti na hapo zamani waliohitimu walikuwa watu wazima zaidi, sababu mojawapo, ikiwa ni kuanza shule ya msingi katika umri mkubwa.

Hatua ya wanafunzi wa shule ya msingi kujiunga na masomo ya shule ya msingi, kuanzia umri wa miaka sita hata mitano kwa shule binafsi, kumeongeza kiwango cha wahitimu wa elimu ya juu kuwa na umri mdogo. Kwenye masomo ya elimu ya juu wengi huutumia uhuru wao visivyo na kuingia hatarini.

Ikumbukwe kundi hilo ndilo limo kwenye changamoto, ikiwamo mabadiliko ya mwili kwa kuingia katika kupevuka na ndipo vishawishi, tamaa huwa vinaambatana na ukuaji huo, hii ikihatarisha malengo ya kundi hilo.

Elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango, bado ipo chini kwa baadhi ya Watanzania, jambo ambalo moja kwa moja linawaathiri zaidi mabinti walio katika umri wa shule.

Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi, Dk. Elias Kweyamba, kutoka Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi Tanzania (AGOTA) na Mhadhiri wa Chuo cha Afya Ifakara, anasema nchini kila mwaka wanawake milioni moja hupata ujauzito, usiotarajiwa.

Anataja miongoni mwao, mabinti walio katika umri wa miaka 15 hadi 19, huingia kwenye kundi hilo la mimba zisizotarajiwa, jambo linalohatarisha mwenendo wao ikizingatiwa wengi wapo ndani ya umri wa masomo.

Hilo linafanyika, huku kuna takwimu zinataja asilimia 22 ya mabinti masomoni wananasa kwenye mimba.

Kwa hali hiyo, bingwa huyo anasema kwa walio wengi hufikia uamuzi wa kutoa ujauzito, kwa njia tofauti huku wanaotoa kwa njia zisizo salama au kwa kutofuata ushauri wa madaktari, wakiwa hatarini.

"Asilimia 39 ya mimba hizo milioni moja huishia kutolewa na huweza kusababisha kuvuja damu sana, kupata maambukizi katika mfumo wa uzazi, ugumba, maumivu makali, fistula na hata kifo," anasema.

Kutokana na takwimu hizo ambazo chanzo chake ni utafiti uliopewa jina la Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Mwaka 2022, uliozinduliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan, ni kwamba katika kundi la mabinti wa umri huo, wapo wanaojihusisha na ngono.

Mbinu anayoitoa bingwa huyo, ni kuongezwa kwa elimu kuhusu afya ya uzazi, ikiwamo ya kupanga uzazi ili kuepukana na mimba zisizotarajiwa na vifo vitokanavyo na uzazi.

Asilimia 13 hadi 16 ya vifo nchini, vitokanavyo na sababu za uzazi huchangiwa na utoaji mimba usio salama, kutokana na mbinu zinazotumika kama vile mazingira duni kinyume na kanuni za afya, anafafanua.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Kweyamba anasema jamii isiwe kikwazo kwa mabinti hao kuamua kutumia njia za uzazi wa mpango, kulingana na wanavyoshauriwa, ili kuepuka vifo.

Unyanyapaa kwa mabinti hao kwa ambao wanaofika vituo vya huduma ya afya ya uzazi, anataja kuwa miongoni mwa sababu wengi wao kutotumia njia yeyote ya kupanga uzazi, wengi wakiangukia katika kundi la mimba zisizotarajiwa kwa wanaojihusisha na ngono.

Anasema wakati umri wa kupekuvuka mabinti hao unapofika, ndipo miili yao inapoanza kuwa na dalili ya kuanza uhusiano wa kingono, bila kuchukua tahadhari, kwa kujikinga kuepuka ujauzito na maambukizi.

Jamii itambue, kwamba, wapo baadhi ya vijana hasa mabinti ambao huanza kujihusisha na mapenzi wakiwa wadogo kwa umri, aidha kutokana na sababu tofauti kama vile kutokuwa na elimu ya afya ya uzazi na kusababisha kutotimiza ndoto zao, hivyo waelimishwe.

HABARI KITAIFA

## Airtel, kampuni za bima waweka mkakati upatikanaji wa huduma

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano ya simu ya Airtel kwa kushirikiana na Bima Jubilee na Axieva, wamezindua huduma ya Afya Bima Kidijitali kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa mtu mmoja au familia.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na kampuni hizo, utaratibu huo unalenga kuleta mapinduzi kwenye bima ya afya kwa kutoa huduma nafuu na zenye kukidhi mahitaji ya soko kwa njia ya Airtel Money.

Kwa mujibu wa utafiti wa Finscope Tanzania wa mwaka huu, ni Watanzania milioni 3.5 pekee wenye bima ya afya kulinganisha na milioni 4.2 waliokuwa nazo mwaka wa 2017.

"Asilimia 75 ya Watanzania ambao wanamiliki simu za mkononi wataweza kufaidika na huduma hii ambayo imetengenezwa vizuri kwa matumizi ya bima ya afya kwa njia ya simu za mkononi.

"Suluhisho hili la Afya Bima litawanufaisha mamilioni ya Watanzania ambao wamekosa huduma ya bima ya afya kutokana na changamoto mbalimbali kama vile upatikanaji wake au urahisi wa upatikanaji wa bima ya afya," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Ilielezwa zaidi katika taarifa hiyo kuwa kutakuwa na mpango wa Afya Poa ambao fedha taslimu zitalipwa kwa mteja ambaye atakuwa amelazwa, fidia ikilipwa kwa kiasi cha kuanzia Sh. 20,000 hadi 50,000 ambayo itahesabiwa kuanzia siku ya pili pale mteja atakapokuwa amelazwa.

Mteja atanufaika na bima hiyo pale tu atapokata bima kwa kiasi cha Sh. 300 kwa siku na Sh. 3,000 kwa mwezi.

"Kutakuwa na Afya Supa, itawapa wateja waliolazwa huduma ya bila malipo pindi wanapolazwa gharama ya matibabu ya hadi Sh. milioni tano na mbili kwa kinamama wanaojifungua kwa mwaka na hii inaweza kumjulisha mwenza, watoto mpaka na wategemezi watano," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Ilifafanuliwa katika taarifa hiyo kuwa mteja atalipia Sh. 15,000 akiwa mwenyewe na Sh. 30,000 akiwa na familia yenye wategemezi wanne na mteja atalipa Sh. 45,000 kwa mwezi kwa wategemezi saba.

"Suluhisho la bima hizi imetengenezwa kuwa jumuishi ikilenga watu wa rika zote kwa umri wa chini wa miaka 18 na wa juu zaidi miaka 65," ilifafanuliwa katika taarifa hiyo.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Beatrice Singano, alisema: "Kwa mara nyingine tunayo furaha kuleta ubunifu wa kipekee kwenye mfumo wa kidijitali wa bima ya afya hapa Tanzania kupitia ubia wetu na kampuni hizi za bima."

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya Jubilee, Dk. Harold Adamson alisema: "Tunayo furaha kuingia kwenye ushirikiano huu kati yetu ya wenzetu Airtel Money pamoja na Axieva ambayo utaleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya bima nchini.

"Tunaleta huduma hizi kubadilisha na kuboresha sekta ya bima ya afya. Tuna bidhaa bunifu kama Afya Poa, Afya Supa na Afya Dhahabu ambazo kila moja ina faida zake ambazo zinalenga kunufaisha mteja pamoja na Watanzania kwa ujumla."

Mkurugenzi Mtendaji wa Axieva Afrika Lab Gaurav Dhingra alisema: "Lengo letu ni kutengeneza mfumo endelevu ambao unaweza kukidhi vyema na kuwezesha jamii kwa kutumia teknolojia."



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la HerInitiative, Lidya Charles (wa pili kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu wa mafunzo maalum ya namna ya bora ya kuomba kazi, ikiwamo uandishi wa barua na jinsi ya kujieleza katika mahojiano ya kazi, yaliyohusisha wanafunzi 60 wahitimu wa kozi mbalimbali katika vyuo nchini na waajiri zaidi ya 25 waliokuja kushuhudia uwezo wa wanafunzi jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajivunia kutekeleza miradi ya mabilioni

**Na Mary Geofrey**

UONGOZI wa Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam umeainisha miradi ya maendeleo inayotekelezwa, ukimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa serikali yake kutoa fedha za utekelezaji wa miradi katika halmashauri hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Eliasi Ntiruhungwa (pichani), amemshukuru Rais Samia kwa serikali yake kupeleka fedha kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi katika sekta mbalimbali.

Ntiruhungwa anabainisha kuwa manispaa ya Ubungo mwaka huu imepata Sh. bilioni 52.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati yake, Sh. bilioni 27.4 zinatumika katika miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa hospitali.

Anasema halmashauri nayo imetenga Sh. bilioni 25.3 kutoka katika mapato ya ndani, zote zikielekezwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mkurugenzi huyo aliishukuru serikali kwa kuwekeza katika sekta ya afya, elimu, uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kutatua changamoto zilizokuwa zinakabili kwa muda mrefu kwa kutoa fedha katika halmashauri kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanapambana na umaskini na wanapata huduma bora, mijini na vijijini.

""Utekelezaji wa miradi hiyo unafuatia dhamira aliyonayo Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu

Hassan ya kuboresha maendeleo na maisha ya wananchi ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi," alisema.

Katika eneo la mipango miji, mkurugenzi huyo anasema halmashauri ina mpango wa kuendesha upimaji na urasimishaji ardhi katika Manispaa ya



Ubungo, mradi utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB).

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imetenga Sh. bilioni 1.3 katika kutekeleza mpango huo ambao maofisa ardhi watapima ardhi na kutoa hati papohapo.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba, anasema wameshaweka mikakati ya ulinzi na usalama katika kuhakikisha wananchi wa wilaya hiyo wanakuwa salama na kushiriki shughuli za uzalishaji mali.

Anasema wilaya imeendelea kuandaa maeneo ya uwekezaji na kuendelea kutafuta wawekezaji katika maeneo mbalimbali, akimshukuru Rais Samia kwa kusaidia kuleta mwekezaji kutoka China.

Wilaya ya Ubungo inaeendelea kuwezesha ujenzi wa kituo kikubwa cha kibiashara Afrika Mashariki na Kati, ambacho bidhaa zilizokuwa zikiagizwa toka nje, sasa zitapatikana katika kituo hicho cha kibiashara cha kimataifa.

Mkuu wa Wilaya pia anaeleza kuwa katika kupunguza kero kwa watumiaji miundombinu ya barabara, wameendelea na utekelezaji wa miradi ya barabara ya kimataifa ya njia nane katika Barabara ya Morogoro ambayo itasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa msongamano wa magari katika wilaya hiyo.

Mstahiki Meya wa Halmshauri ya Ubungo, Jafary Nyaigesha, anasema fedha zinazotolewa na serikali zinatumika vizuri kutekeleza miradi na uboreshaji wa huduma za elimu, afya na mingineyo yenye maslahi kwa umma.

Anasema Baraza la Madiwani limejipanga kuhakikisha fedha zote zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi katika Manispaa ya Ubungo zinatumika vizuri na kufikisha huduma zilizokusudiwa ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Ofisa Elimu ya Awali na Msingi, Mwalimu Denis Nyoni na Ofisa Elimu Sekondari, Mwalimu Voster Mgina, walieleza jinsi walivyojipanga kuhakikisha wanasimamia vyema miradi ya elimu na fedha za serikali zinazotolewa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na zile zinazotokana na mapato ya ndani ya halmashauri, kukitekelezwa miradi ya mabilioni katika maeneo yao ya kazi.

Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Mary Mwakyosi anasema kuwa serikali chini ya Rais Samia, imekuwa mstari wa mbele kuboresha mazingira ya kibiashara na kuvutia uwekezaji, ikijenga masoko mapya na kukarabati yaliyopo.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Ubungo, Dk. Tulitweni Mwinuka anasema manispaa imefanikiwa kuboresha sekta ya afya kupitia ujenzi wa miundombinu na kuongeza watumishi wa afya, vifaa tiba na dawa katika vituo vya afya.

# Waziri: Tulinde viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo amesema kuna haja ya kuwalinda wawekezaji wa ndani dhidi ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwa kuweka sheria itakayokuwa na mizani ya usawa.

Amesema wawekezaji wengi wa ndani wanazalisha bidhaa zenye ubora, lakini wanakabiliwa na ushindani na bidhaa zinazotoka nje.

Alitoa angalizo hilo jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kwanza cha kuunganisha magari madogo nchini kinachotarajiwa kuwekeza zaidi Sh. bilioni 10.

Uwekezaji wa kiwanda hicho ni ushirikiano kati ya kampuni ya GF Automobile na Mahindra kutoka India. Umefanyika siku 25 tangu Rais Samia Suluhu Hassan azuru India kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini.

Prof. Kitila alisema kampuni hiyo imekuja kwa hatua ya kwanza na ndani ya miezi sita ijayo wataanza kuzalisha magari hayo nchini.

Alisema," uwekezaji huu utawapa fursa ya ajira vijana wetu, kodi kwa serikali na kuongeza uchumi kwa Watanzania na Taifa kwa ujumla."

Alisema uwekezaji huo unakwenda sambamba na malengo ya serikali katika kuvutia wawekezaji wa magari nchini hasa yanayotumia umeme.

Mkurugenzi wa GF Group, Imran Karmali alisema kuanza kwa uunganishwaji magari hayo madogo nchini kutasaidia kushusha gharama za uagizaji na kuwafanya Watanzania kumudu gharama.

"Magari haya yatakuwa mapya. Hivyo kama malengo ya serikali ni kusaidia viwanda vya magari viongezeke, ni vyema kuweka mazingira magumu kwa magari yaliyo na miaka mingi kuingia nchini," alisema.

Aliongeza kuwa waliona fursa ya kushirikiana na Mahindra baada ya Rais Samia kutembelea India, wakatafuta kampuni kutoka nchini humo ili washirikiane nao.

Alisema kampuni ya GF imekuwa moja ya kampuni zinazounganisha magari makubwa nchini kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo kubeba mizigo na kwa mwaka huu pekee hadi Oktoba walizalisha zaidi ya magari 1,000.

"Tunapokwenda kuanza uzalishaji wa magari madogo, tutaongeza pia idadi ya ajira zitakazozalishwa, kwa sasa watu 250 wameajiriwa huku 700 wakiwa ajira zisizokuwa rasmi," alisema Karmali.

Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri alisema ujio wa kampuni hiyo unaakisi ongezeko la uwekezaji lililoshuhudiwa kati ya Julai hadi Septemba mwaka huu ambapo mtaji wa zaidi ya Sh. trilioni 2.505 umewekezwa sekta mbalimbali.

Alisema uwekezaji huo ni mara mbili ya kile kilichokuwapo kipindi kama hicho mwaka 2022, pia ni nusu ya uwekezaji ambao Tanzania iliupata kwa mwaka 2019 na 2020.

Hivyo, aliwataka Watanzania kushiriki katika mageuzi ya kiuchumi kwa kutumia vivutio mbalimbali vilivyowekwa na serikali kwa ajili yao ili wawekeze kwa urahisi zaidi na kupata ushirikiano.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (kulia), akipata maelezo kutoka kwa wawakilishi wa International Youth Fellowship inayojihusisha na shughuli za kujitolea alipotembelea banda la shirika hilo, wakati wa maadhimisho ya 52 ya Siku ya Kimataifa ya Kujitolea (IVD), jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Prof. Ndalichako awapa mbinu wanaosaka ajira

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, ameeleza umuhimu wa kujitolea kusaidia taifa katika maeneo mbalimbali.

Katika maadhimisho ya 52 ya Siku ya Kimataifa ya Kujitolea (IVD), akimwakilisha Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa jijini Dar es Salaam juzi, Prof. Ndalichako alisema:

"Hata mimi nilijitolea, nikaanza kupata 'maokoto' (fedha) lakini pengine nisingeweza kujitolea huenda nisingejulikana, maana nianza kujulikana kupitia kujitolea.

"Ndugu zangu, kujitolea kuna faida, si lazima uanze kupata fedha hapohapo."

Waziri huyo alisema suala la kujitolea ni muhimu kwa kuwa linasaidia kupunguza uhitaji uliopo wa rasilimali watu inayohitajika katika kutekeleza majukumu yao.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote wanaohusika na masuala ya kujitolea ili kukuza na kuunganisha nguvu ya kujitolea katika kuelekea dira ya matumaini na msukumo wa kujitolea kwa Watanzania.

"Kwa kuwa sisi Watanzania ni kitovu katika ukanda wa unaohusisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tutashirikiana na nchi wanachama wa jumuiya hii na nchi zingine jirani ili kukuza utamaduni thabiti wa kujitolea kuelekea kufikia ustawi kwa wote katika ukanda huu wa Afrika Mashariki," alisema.

Waziri huyo pia alisema tangu uhuru wa nchi, wananchi wake wamejenga tabia ya kujitolea kupitia njia mbalimbali ikiwamo ujamaa, utaratibu ambao watu waliishi na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote.

"Hata leo hii, Watanzania wanaendelea kutoa michango yao mingi na mikubwa kupitia vipaumbele mbalimbali vya maendeleo ya taifa nchini, jambo ambalo linaunga mkono mipango mbalimbali ya kimaendeleo inazofanywa na serikali na mashirika ya kiraia," alisema.

# Kukosekana ushindani kutadumaza biashara

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema kukosekana ushindani kutadumaza soko la biashara la ndani, hivyo kuna haja Tume ya Ushindani (FCC) kusimamia kikamilifu sheria na kanuni za ushindani kwenye biashara.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji aliagiza hayo wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ushindani Duniani yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Aliitaka FCC kuendelea kufanya kazi zake kwa uadilifu na kuwezesha wafanyabiashara kufanya biashara zao kihalali ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Madhumuni ya serikali si kukataza biashara, bali kuweka mazingira mazuri ya kufanyia biashara. Wenzetu FCC wana wajibu wa kusimamia sheria zote za ushindani.

"Kwa sasa nchi yetu imefunguka kwenye ushirikiano wa biashara na nchi nyingine, wawekezaji wanazidi kumiminika, hivyo lazima tuimarishe mazingira ya kufanyia biashara," alisema Dk. Kijaji.

Alisema kwa sasa lazima Tanzania ijipange na kuangalia namna ya kushindana katika soko la kimataifa.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha, Dk. Kijaji ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya FCC, Dk. Aggrey Mlimuka, alisema wafanyabiashara hawana budi kutii sheria za ushindani na biashara.

Alisema tayari tume hiyo ina maombi ya muunganiko wa kampuni 28 zenye thamani ya Sh. bilioni 700 na tume hiyo itasimamia ushindani kwa haki.

"Tutatekeleza maagizo yote tunayopewa na serikali, hatutakubali kuwa na mtu atakayetukwamisha katika utekelezaji wa majukumu ya tume hii, biashara zinafanyika kwa kufuata sheria na ushindani unakuwapo," alisema Dk. Mlimuka.

Mkurugenzi Mkuu wa FCC, Dk. William Erio, alisema maadhimisho hayo yanafanyika Desemba 5 kila mwaka na kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Njama Baina ya Washindani na Madhara Yake kwa Mlaji'.

Alisema tume hiyo imetoa semina kwa makundi mbalimbali kuhusu uelewa wa ushindani na shughuli za tume hiyo.



# Wafanyabiashara madini wapongeza kurejeshwa maonyesho ya kimataifa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wa madini mkoani Arusha, wamesema wameridhishwa na mpango wa serikali kurejesha upya maonesho na minada ya kimataifa ya madini.

Walisema hatua hiyo itakuwa chachu ya kukuza uchumi wa nchi na kuongeza kipato kwa wafanyabiashara kupitia sekta hiyo kwa kuwa watakuwa na nafasi kubwa ya kunadi bidhaa zao moja kwa moja kwa wateja.

Akizungumza na Nipashe jana kwa niaba ya wafanyabiashara wa madini mkoani humo, Mwenyekiti mstaafu wa Chama cha Wafanyabiashara, Wanunuzi na Wauzaji wa Madini Tanzania (TAMIDA), Sammy Mollel, alisema hatua hiyo itaisaidia sekta hiyo kupiga hatua nchini.



"Sisi kama wafanyabiashara tunaona kitendo cha Serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (pichani) kurejesha maonesho na minada kizuri ambacho kimeangalia maslahi ya nchi kwa kuwa itaendelea kifungua milango ya kibiashara katika sekta hiyo," alisema Mollel.

Alisema tangu serikali ilipopitia na kufumua Sheria za madini na kusitisha maonesho na minada hiyo kwa muda mwaka 2017 mambo mengi yalisimama na kukwama.

Aidha alisema maonesho na minada hiyo inafaida nyingi kwa wafanyabiashara kwa kuwa yatawashirikisha itawakutanisha na wenzao kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Pia alisema yataleta faida nyingi kwa nchi kwa kuwa yanafanyika hapa nchini mkoani Arusha, taifa linapata fursa ya kutangaza rasilimali za madini zilizoko nchini.

"Kwa wanunuzi wakubwa duniani wanapata nafasi ya kukutana ana kwa ana na wazalishaji wetu wa madini, kuketi meza moja kufanya biashara na hatua hiyo inawajengea ujasiri wazalishaji wazawa na kujitengenezea mtandao wao,"aliongeza.

Vilevile alisema vyama vya wanunuaji wa madini vitapata fursa ya kubadilishana uzoefu na vyama vya madini vya kimataifa kwa ajili ya kutangaza rasilimali hiyo.

# Kilichojificha viongozi wa dini kuchelewa kukemea ukatili

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MGOGORO wa maduka ya biashara kati ya Halmashauri ya Jiji la Arusha na wafanyabiashara walioyajenga katika eneo la stendi ndogo, limechukua sura mpya baada ya viongozi wao kushikiliwa kituo cha polisi na kutakiwa kutoa maelekezo.

Viongozi hao wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Mkoa wa Arusha, Lokeni Masawe, walipigiwa simu ya wito kwenda Kituo cha Polisi wakati wakiongoza mkutano wa wafanyabiashara waliojikusanya eneo hilo kujadili sakata hilo.

Viongozi wengine walioitwa ni Mwenyekiti wa wafanyabiashara Wilaya, Dominic Mollel na Mwenyekiti wa maduka ya stendi ndogo, Lorandi Kwayu.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao Wilaya ya Arusha, Dominic Mollel,alikiri kuitwa Kituo cha Polisi na kuhojiwa kwa zaidi ya saa tatu juu ya mikataba ya ujenzi wa vibanda hivyo na baadaye walidhaminiwa.

Hivi karibuni Mkurugenzi wa Jiji hilo, Juma Hamsini, alitishia kuvipiga mnada vibanda vya wafanyabiashara hao kwa watu wengine iwapo wafanyabiashara wajenzi wataendelea kukaidi kujisajili mikataba mipya yenye ongezeko la pango kutoka Sh.200,000 hadi Sh.250,000.

Wafanyabiashara hao, waligomea utaratibu wa Mkurugenzi huyo,wakidai kuwa wao ni wajenzi na wanapaswa kutambulika kama wamiliki halali wa vibanda na sio wapangaji, hivyo hawapaswi kujisajili kama wapangaji kupitia mfumo mpya wa ukusanyaji mapato ya serikali wa TAUSI.

Akizungumza katika mkutano huo, Katibu wa Wafanyabiashara hao, Angelus Shokia, alimwomba Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuingilia kati mgogoro huo ambao unahali mbaya za kufifisha mapato ya serikali.

Hata hivyo, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikikusanya mapato kutoka kwenye vyanzo hivyo zaidi ya Sh.milioni 900 kwa mwaka na wanashangaa kutaka kuwapoka vibanda hivyo.

Alisema mgogoro huo umekuwa ukiibuka mara kwa mara hasa kunapokaribia uchaguzi na Waziri Mkuu aliwahi kuingilia kati na kuzuia utoaji wa mikataba mipya na kubariki wafanyabiashara hao kuendelea kumiliki vibanda hivyo kama wajenzi bila kubughudhiwa.

"Hili jambo limekuwa likijirudia mara kwa mara, mwaka 2016 Waziri Mkuu Majaliwa aliingilia kati na kutoa maelekezo kupitia barua aliyoitoa Desemba 3, 2016 na nakala kupelekwa kwa Mkurugenzi Jiji la Arusha na kwa katibu Tawala Mkoa wa Arusha,"alisema.

Shokia alisema, katika miaka tangu mwaka 1990 wafanyabiashara hao waliingia makubaliano na halmashauri hiyo,kujenga maduka hayo huku halmashauri ikimiliki ardhi na wao walimiliki maduka hayo kwa muda usio na kikomo.

Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Juma Hamsini, aliwataka wafanyabiashara hao kufuata utaratibu wa serikali ikiwemo kujaza fomu za mikataba mipya na kujisajili kupitia mfumo wa TAUSI.


## Lindi Jumbo Limited
TANZANIA

Lindi Jumbo Limited

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR PROVISION OF CAMP MANAGEMENT AND CATERING SERVICES REFERENCE NO LJL-2023-005 LINDI JUMBO GRAPHITE PROJECT**

The Lindi Jumbo Graphite project is situated in southeastern Tanzania, about 200 km away from the port of Mtwara. The project area can be accessed from the southern part via sealed roads that lead from Mtwara to Nanganga, which is approximately 15 km to the north of the town of Ruangwa. Lindi Jumbo Limited (The Company) is seeking a qualified camp management and catering provider for the company's graphite mine project, commencing operations in January 2024. The project will involve a team of approximately 85 camp residents.

**BRIEF DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE SERVICES:**
This scope of work aims to outline the specific responsibilities and requirements for exploration camps and refurbished sea container providers ("The Contractor").

**A. Objectives:**
The primary objectives of The Contractor are as follows:
i. Manage and supply catering services in a functional camp in the Ruangwa region
ii. Ensure the team members' well-being and comfort during their camp stay.
iii. Provide necessary logistical support to enable efficient operations and smooth functioning of the mining project.
iv. Maintain compliance with local laws, regulations, and environmental guidelines.

**B. Contractor's responsibility for Camp Management and Setup:**
i. Develop a comprehensive camp management plan, including infrastructure requirements, layout, and facilities.
ii. Procure and install industrial catering equipment sufficient for the number of camp residents.
iii. Provide full-time on-site management and supervision of the camp throughout the duration of the project.
iv. Assign dedicated staff members for camp operations, including cooks, maintenance team, housekeeping staff, and grounds staff.
v. Maintain a clean and hygienic camp environment, including regular waste management and cleaning services.
vi. Manage food and catering services, ensuring the provision of nutritious meals for the team as per dietary requirements.
vii. Establish a system for laundry services to ensure team members have clean clothes and bedding.

**C. Logistics and Support and Local Content:**
i. Arrange transportation services for camp staff.
ii. Coordinate with local suppliers to procure necessary equipment, materials, and supplies for the project within local content regulations.
iii. Establish a system for inventory management to ensure adequate stock of essential items.
iv. Arrange necessary OSHA permits and other logistical support as required.
v. Ensure, where possible, that general labour from the local community is hired.
vi. Work with The Company to identify the amount of general labour.
vii. Where possible, purchase locally.

**D. Health and Safety:**
i. Participate in a formal risk assessment with The Company prior to camp setup.
ii. Implement appropriate health and safety measures in line with the company's protocols to mitigate risks and ensure the well-being of all team members.
iii. An Emergency Management plan is implemented and tested.
iv. Provide The Company with necessary safety protocols and camp management plans.
v. Conduct camp orientations and inductions to all new arrivals.
vi. Camp staff will participate in morning pre-start meetings.
vii. Make use of NCAP 5-star vehicle for supporting the camp.

**MINIMUM REQUIREMENTS:**
1. Proof of registration with the Tanzania Revenue Authority (TRA).
2. Company Information - including but not limited to corporate details, trading name, company registration number, official report from BRELA, Local Content Compliance, and Tax Clearance Certificate for the latest year.
3. Company profile.
4. Capability Statement.
5. Copy of certificates of accreditation with other operations.
6. List of Insurances, where applicable.
7. Quality Assurance Plan.
8. Monthly cost operations

Companies that have the ability, capacity, and resources to implement the services listed above should express their interest by uploading their proposals via the Procurement portal, **www.webportunities.net** only proposals submitted via the portal will be evaluated. All documents must be submitted in English on or before 24:00hrs East African Time (EAT) on **20th December 2023.** If you require assistance on the portal, please contact the Tara Nawa team via the portal's Contact Us page.

Lindi Jumbo Limited will review and assess the documents provided by companies that have expressed interest in accordance with this EOI and conduct evaluations based on internal criteria to determine which companies will be included in the list of pre-qualified companies. Only the pre-qualified companies will receive, by signing a Non-Disclosure Agreement (NDA), an invitation to bid as a continuation of the call for tender process.

Lindi Jumbo Limited is not bound to accept the lowest or any tender offer received, and the adjudication of the tender will be based solely on the discretion of the company with consideration given to both qualification and commercial aspects.

217744402





# TANAPA yaondoa tembo waliovamia Kyerwa

**Na Jenesta Jasson,** KYERWA

ASKARI wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) wamefanikiwa kuyaondoa makundi ya tembo walikuwa wamevamia maeneo ya vijiji vitano vilivyoko katika Kata ya Businde wilayani Kyerwa mkoani Kagera kwa zaidi ya miaka 10.

**Tembo hao wameswagwa hadi umbali wa kilomita zaidi 45 kutoka katika maeneo ya vijiji hivyo na wana matumahini kuwa hawatarudi.**

Hali hiyo ilisababaisha kaya zaidi ya 50 kuhama katika vijiji hivyo kunusuru maisha ya familia zao kutokana na hofu ya tembo hao walioanza kuwashambulia na kuwaua na kuharibu makazi na mazao yao.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa, Kamishna wa Uhifadhi Dk. Fredrick Mofulu, alisema operesheni ya kuondoa tembo hao ilichukua siku tano katika vijiji vya Nyakashenyi, Businde, Kibare, Bugara na Kijumbura na kwa sasa tayari wamedhibitiwa.

Alisema tembo hao wameswagwa hadi umbali wa kilomita zaidi 45 kutoka katika maeneo ya vijiji hivyo na wana matumahini kuwa hawatarudi vijijini humo na njia zao za kuingilia ni tatu tayari zimewekewa ulinzi.

Vilevile alisema tayari wameanzisha mpango wa kutoa mafunzo kwa vijana wa vijiji hivyo juu ya namna ya kuwadhibiti tembo hao yatakayotolewa na Chuo cha Wanyamapori cha Pansiasi kilichoko mkoani Mwanza.

Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Zaitun Msofe, alishukuru kwa kazi kubwa iliyofanywa na askari hao kwa kuwa walikuwa kero kubwa kwa wananchi na sasa wataishi kwa amani na utulivu.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar, Fedha na Mipango, Jamal Kassim (wa pili kushoto), akikabidhi tuzo kwa Mkuu Kitengo cha Ukaguzi Hesabu za Ndani wa Benki ya Exim Tanzania, Colman Riwa, baada ya benki hiyo kuwa miongoni mwa benki tatu bora katika uandaaji wa Taarifa za Fedha ya Mwaka 2022 kwa taasisi kubwa zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Sylivia Shayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Atuhumiwa kuiba mtoto wa bosi wake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kijiji cha Igundu, Kata ya Mwalugulu, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, Dotto Said (25), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuiba mtoto wa mwajiri wake mwenye umri wa miezi sita na kumpeleka mkoani Tabora kwa mpenzi wake.

Akithibitisha kukamatwa kwa binti huyo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema baada ya kuhojiwa alidai kuwa mama wa mtoto alikubaliana naye.

Alisema mtuhumiwa huyo alidai walielewana na mzazi wa mtoto ili akamdanganye mpenzi wake Nzega kwa kumwonyesha mtoto huyo kwani hapo awali alikuwa akimhadaa kuwa ni mjamzito.

Alisema kwa sasa mtuhumiwa huyo amewekwa chini ya ulinzi wakati upelelezi unaendelea chini ya mkuu wa kituo cha Kagongwa ili kubaini ukweli wa tukio hilo.

Doto Saidi alikuwa ameajiriwa na Elizabeth Joseph (37) kufanya kazi saluni iliyopo Mtaa na Kata ya Kagongo na siku zote alikuwa akimhadaa mpenzi wake kuwa ni mjamzito na kupewa matumizi huku ikiwa sio kweli.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kagongwa, Michael Shija, alisema Desemba mbili, mwaka huu majira ya saa tano asubuhi walipokea taarifa ya kuonekana kwa binti huyo na saa 12 jioni walitoa maelekezo kwa walinzi wa jadi 'Sungusungu' na kuanza kumtafuta.

Alisema, askari hao walianza kumtafuta kwa kutumia picha ya pacha wake, Kulwa Saidi, na walipompata alimpigia simu na kumweleza kuwa yupo Nzega mkoani Tabora kwa mpenzi wake hivyo kumfuata na kumkamata akiwa na mtoto huyo katika eneo la Uchoma.

Mama wa mtoto huyo, Elizabeth Joseph, alisema baada ya kumaliza kumnyonyesha mtoto wake aliombwa na mfanyakazi wake kumbeba na kwenda naye dukani na hakuwa na hofu kwa kuwa ni mtu aliyemzoea.

Alisema baada ya kuondoka alimsubiri bila kurudi, kisha akampigia simu na kumwambia anamleta mtoto lakini hakufanya hivyo, ilipofika jioni akaamua kutoa taarifa kwa uongozi wa mtaa.

Shuhuda wa tukio hilo, Regina Selemani alisema, kila siku alikuwa akimsikia Dotto akizungumza kwenye siku na mpenzi wake kuwa ni mjamzito na muda wowote angejifungua na alijua anafanya utani kwa lengo la kumchukulia fedha mpenzi wake.

Kiongozi wa Sungusungu Mtaa wa Kagongwa, Ndaki Daudi, alisema vitendo vya wizi wa watoto katika kata hiyo vimeshamili sana. Tangu mwaka 2020 mpaka sasa kuna matukio zaidi ya sita ya wizi wa watoto yameripotiwa, kati ya hayo ni moja tu ambalo mtoto kapatikana.

## TRA yakumbushwa kuzingatia agizo la Rais ukusanyaji kodi

**Na Waandishi WetU**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Kanda ya Ziwa imehitimisha kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Mlipakodi wakikumbushwa kuzingatia agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kufuata taratibu za kisheria katika ukusanyaji kodi.

Agizo lililotolewa na rais ni la kuweka utaratibu mzuri wa kuwabana wafanyabiashara kulipa kodi na si kutumia nguvu ikiwamo kufunga maduka yao bila utaratibu maalum.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, wakati wa hafla ya kilele hicho katika mkoa huo na kuiagiza mamlaka hiyo kuwekeza zaidi katika kutoa elimu ya mlipakodi ili kuongeza walipaji kodi.

"Fanyeni makadirio sahihi ya kodi ili kutowaumiza wafanyabiashara kwani wanapitia mengi kuanzisha biashara hizo, kufunga biashara siyo jambo zuri, mtu anajitoa mhanga anakopa anafungua biashara lakini mtu tu hata siyo TRA anasema funga biashara, suala hili mlitizame sanaa," alisema Makalla.

Aidha, Makalla aliipongeza mamlaka hiyo kwa kuvuka lengo na kukusanya mapato ya Sh.bilioni 269.78 ikiwa ni pamoja na kuitumia wiki ya mlipakodi kusaidia wenye uhitaji.

Alitaja misaada iliyotolewa kuwa ni shuka 128, neti 128, baiskeli mbili za wagonjwa, themometa 50, taulo za watoto, dawa za meno na vifaa vya usafi vyenye thamani ya sh. milioni sita vilivyokabidhiwa kwa Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana.

Katika hatua nyingine Makala alieleza mwelekeo na dira ya jiji la Mwanza katika kukusanya mapato pamoja na mipango ijayo ya serikali ikiwa ni pamoja na kuidhinishwa kwa Sh.bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kisasa la abiria katika uwanja wa ndege wa Mwanza.

**Imeandikwa na Rose Jacob (MWANZA), Thomas Wandiba (SAUT) ,Jenesta Jasson ( KAGERA)**

ama
ALHAMISI DESEMBA 7, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

## PROGRAMU VITA UTAPIAMLO 2021/22 - 25 Samia vitani, bajeti halmashauri kwa kila aliye taabani; ajira maofisa lishe



## SIMULIZI YA BINADAMU ALIVYOTOKEA KWENYE UMBILE NA AFYA YA SOKWE

Ukurasa 13

### AWAMU YA SITA NA MAPINDUZI JINSIA

# GDP 3.5% yawekezwa kukabili 'wakatili', wanaowapa mimba 22% walioko shuleni

## •Marufuku ulazima mume kliniki...abembelezwe

**Na Yasmine Protace**

KUNATAJWA haja ya kutolewa elimu kwa wanandoa, ili wajenge utamaduni wa kuongozana kliniki ya wajawazito na watoto, wakiwa wameambatana na wenza wao.

Ni kauli ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kwa wanandoa na wasio wanandoa, pia inagusa jamii, ili isaidie kila mwenye ujauzito asiye na ndoa au aliye na ndoa, aambatane na mwenza wake katika kliniki ya wajawazito na watoto kwa hiari.

Hata hivyo katika uhalisi, inaelezwa kwa baadhi ya jamii kwa kutokuwa na elimu hiyo, wamekuwa wakishangaa kuona mwanaume akimleta mtoto kliniki bila ya kuambatana na mwenza wake.

Mfumo dume bado unalalamikiwa kujenga saikolojia kuwa ni jukumu la mama na sio baba.

Lakini sasa, kuna mageuzi yanatajwa baadhi ya wanaume kuwa bega kwa bega na wenza wao, kwa kuongozana nao kliniki mpaka hatua anapojifungua.

Hiyo ni kutokana na baadhi ya wanandoa na wasio wanandao kushindwa kuhudhuria kliniki ya wajawazito na watoto, wakiwa na wenza wao, sasa kuna mtazamo mpya umezaliwa.

Ni zao la hali iliyopawa baadhi yao wamekutana na vikwazo, kwa mama mjamzito anapoenda kliniki ya mama na mtoto.



Vijana wenye watoto kwenye moja ya mahafali, wakiwa wazazi. **PICHA: MTANDAO**

Waziri wa Afya Ummy anatamka katika Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili Kijinsia yaliyofanyika jijini Tanga, kwamba: "Tusiweke vikwazo kwa wanawake ambao wamepata ujauzito na wanaenda kliniki bila ya wenza wao kupata huduma.

"Tuwashauri na tuwape elimu ili waende na wake zao lakini tusiwanyime huduma sababu hawakwenda na wenza wao."

Anaongeza kuwa wanawake wengi wanapewa ujauzito na wanaachwa na wanaume wakihangaika peke yao, hivyo si sahihi kuwamlazimisha waende bila ya wanaume.

Ummy anaongeza kuwa, ni marufuku kulazimisha mwanamke mjamzito kwenda na mwenza wake kliniki, ili kupata huduma.

"Hii imechangia wanawake wanatafuta bodaboda au mwanaume yeyote ampeleke kliniki ili apate huduma hii haikubaliki," anatamka Waziri.

Anafafanua kwamba, inapaswa wanaume wahamasishwe, wapewe elimu kuwa hilo ni muhimu baba na mama wote wakaenda kwa pamoja wakaenda kliniki, lakini sio kuwalazimisha wanawake.

Vilevile Waziri Ummy anasema, jamii ina wajibu wa kuzuia vitendo vya ukatili wa jinsia, kukabiliana kuzuia mimba za utotoni.

Anasema kuzuilika kwa matukio hayo ya ukatili, kutawasaidia watoto wa kike kusoma na kutimiza ndoto zao.

"Mimba za utotoni ni asilimia 22, yaani katika kila watoto wa kike 100, watoto 22 wanapata ujauzito katika umri mdogo," anasema.

Anaongeza kuwa ni jukumu la madaktari wote nchini kuacha kuogopa kutoa taarifa sahihi za vitendo vya ukatili, kama mtoto amebakwa aseme na kama mtoto ameingiliwa kinyume na maumbile aseme, kwa kuwa hatovumilia mtu yeyote atakayeficha ukweli kuhusu vitendo vya kikatili.

"Serikali haitomvumilia mtu yeyote wa ubakaji na walawiti wa watoto, madaktari nawasisitiza msiogope kutoa taarifa sahihi kuna baadhi wanaogopa kutoa taarifa za kweli.

"Msiogope, polisi kazi yao ni kutafuta ushahidi, sasa mnapoogopa kutoa ushahidi, mnachangia kuendeleza ukatili wa kijinsia kwa watoto," anasema Ummy.

Pia anawaelekeza wakuu wa wilaya na mikoa kuzingatia maelekezo ya serikali, ikiwamo kuhakikisha kila shule ya msingi na sekondari inakuwa na walimu wa malezi, watakaokuwa kimbilio la watoto kueleza matatizo ya ukatili wanayofanyiwa shuleni na nyumbani.

Waziri Ummy akiendelea kutoa athari za vitendo vya ukatili wa kijinsia, anasema Tanzania inatumia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia, fedha ambazo zingeweza kutumika kwenye masuala ya afya na maji, pia elimu ya watoto hao.

Waziri Ummy amewahakikishia Watanzania kuwa serikali chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, itaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria, ili kupambana na ukatili wa kijinsia, hususani kwa wanawake na watoto.

Balozi wa Ireland nchini, Mary Oj'Neill anaipongeza Tanzania na kuahidi kuendelea kuunga mkono jitihada za kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

AFYA

## PROGRAMU VITA UTAPIAMLO 2021/22 - 25/26

# Samia vitani, bajeti halmashauri kwa kila aliye taabani; ajira maofisa lishe

- TARI yabeba jukumu kuandaa aina ya mlo wao
- Manyara mfano, 'mguu kwa mguu' kieleweke



Mfano wa sehemu ya lishe bora anayopaswa kupata mtoto, iliyotolewa na tovuti ya Hospitali ya Mkoa Manyara. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Jaliwason Jasson,**

**MANYARA BABATI**

NI darasa na ufafanuzi linaloanzia kwa Ofisa Lishe Mkoa wa Manyara, January Dalushi, kwamba sasa kuna mpango mkakati kuboresha lishe na vita dhidi ya utapiamlo mahali hapo.

Anautaja ni mwitikio wa hatua ya serikali mwaka 2010/2011, ilipobuni mpango mkakati wa miaka mitano wa lishe, chini ya Rais Jakaya Kikwete, aliyetoa maelekezo kuanzishwa dawati la lishe, nguvu kubwa ikafanyika kufikiria vyanzo vya fedha kusaidia watoto wenye utapiamlo.

Rais Dk. Samia katika zamu yake kwa hadhi ya 'mama', akatilia mkazo zamu yake, paeleweke kwa kuandaa programu inayoendelea kuchachama katika jamii, mara kadha akijitokeza kuhamasisha mwenyewe juhudi kama alivyoshudiwa mkoani Njombe, ambako hali si ya kuridhisha kwenye lishe.

Ofisa lishe huyo wa Manyara, anasimulia mzizi, pale Wizara ya Fedha ikatoa miongozo ya kibajeti kutoka vyanzo vya ndani, halmashauri zikitakiwa kuangalia ukubwa wa tatizo lilivyo, ili kuokoa watoto.

Anasema, katika mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka 202, zama zake Rais Dk. Samia akiwa Makamu wa Rais, serikali ikatengeneza Mpango Jumuishi wa Kitaifa kuwa na idara zote mtambuka; Afya, Kilimo, Mifugo, Maendeleo ya Jamii, Elimu, Mipango na Utawala na Rasilimali Watu, katika lililoshughulikia hilo, hata kugunduliwa utapiamlo katika jamii.

Kisa chake kikatajwa ni uchumi mdogo katika familia unaosababisha kukosekana chakula cha kutosha, hivyo ni muhimu halmashauri zinapaswa kutenga bajeti kuziba pengo hilo.

### UTEKELEZAJI ULIVYOANZA

Ofisa Lishe, anasimulia mwaka wa fedha 2020/2021 halmashauri zote zilitenga fedha kulingana na idadi ya watoto waliyo nao.

Mkoani Manyara, anasema ujumla yake mwaka huo halmashauri zote zilitenga fedha kwa asilimia 73.47 ambazo zilienda kutekeleza shughuli mahususi.

Anataja shughuli hizo kuwa ni lishe duni, upungufu wa madini kwa watoto chini ya miaka mitano na wanawake wenye umri wa kuzaa, uzito uliozidi na vilibatumbo, uwezeshaji na ufuatiliaji wa shughuli za lishe.

Mtaalamu huyo anasema, fedha zilizotoka vituo vya kutoa huduma na fedha za Mfuko wa Afya, pamoja nazo zinapangiwa kazi za lishe.

Anasema kwa mwaka wa fedha 2021/22, walipanga fedha kulingana na idadi ya watoto na kuzitumia kwa asilimia 50.88, akinena matumizi yanaangukia kuwapa wataalamu kudhibiti utapiamlo usitokee, kila mtoto kutengewa Sh. 1,000 katika halmashauri hiyo.

Kwa Mkoa wa Manyara, anataja halmashauri zake zilitenga fedha hizo, ila hazikufikia makusanya ya asilimia 100.

### OFISA LISHE AELEZA

Dalushi anasema, katika halmashauri kuna vipaumbele vingi, ndio maana wanakusanya chini ya matarajio yao waliyolenga.

Anasema ili kufanikiwa, fedha za mapato ndani ya vituo vya kutoa huduma katika halmashauri, yanatoka kwenye vyanzo tofauti na huduma.

"Vituo navyo tumevielekeza vitoe kipaumbele kwenye lishe, maana tunajua asilimia 50 ya mapato yao zikanunue dawa," anasema Dalushi.

Aidha, anasema asilimia nyingine zifanye shughuli nyingine ikiwamo lishe na mwaka wa fedha 2024/25, anadai watawaelekeza maofisa watendaji wa kata na vijiji kutenga fedha za lishe kupitia mikataba yao watakayoingia, ili ziweze kuja kusaidia wiki ya lishe ambayo inatumika kutoa elimu maeneo ya vijijini.

Ofisa Lishe huyo anawashukru wadau wa maendeleo wanaosaidia eneo la lishe, wakiwamo taasisi za kigeni akitaja baadhi; US Afya Yangu, wanaosaidia mama na mtoto, vilevile Shirika la Global Alliance for Improved Nutrition, watumishi wakijengewa uwezo na matibabu kwa watoto wanaobainika kupata utapiamlo.

Inafafanuliwa, katika baadhi ya halmashauri hazikuwa na Dawati la Lishe, hata kufika hatua Ofisa Kilimo wa wilaya nje ya mkoa, ndiye anapahudumia lishe.

### MAPINDUZI MANYARA

Kwa mujibu wa mtaalamu Dalushi, ikafika hatua katika mwaka wa fedha 2010/2011, serikali ikatoa maelekezo kuanzishwa dawati la lishe, maana awali hakukuwapo muundo wa kuwaajiri maofisa lishe.

Anasema, Mkoa wa Manyara sasa una maofisa lishe 16, akinena inawapa nguvu kuwavusha katika vita kukomesha utapiamlo mkoani.

Anataja katika mwaka 2004, suala la udumavu mkoani humo ulikuwa asilimia 39 wakati mkoa ndio umeanza na sasa utafiti mpya wa mwaka huu wa Tanzania Demographic Health Survey (TDHS), anataja udumavu Manyara ni asilimia 32, akiamini nguvukazi itasaidia kupiga hatua ndani ya miaka mitano, kukiwapo mabadiliko makubwa.

### MALENGO YALIYOPO

Dalushi anafafanua malengo yaliyoko, wanataka wafike asilimia 24 baada ya miaka mitano, kwani hata mwanzoni waliangukia kutibu.

Mtaalamu wa Lishe, anasema Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Mwaka 2021/22-2025/26, wakaona kuna kundi liliachwa na wanahangaika - watoto chini ya miaka mitano na wajawazito, mpango utaangalia namna ujao utagusa makundi yote.

"Tutaangalia maisha ya binadamu wote na tutaelekeza nguvu katika jamii ili wapate elimu ya kutosha,"anaeleza, wakiwa na jukumu la

kutembelea kaya na wakiwa na vifaa sahihi kutambua afya za watoto na uwapo wa utapiamlo.

### VIONGOZI WA MKOA

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) wiki mbili zilizopita, anasema uamuzi wa kutengwa bajeti ya Sh. 1,000 kwa kila mtoto kuhudumia lishe kwao si la kujadili, ni jambo la kutekelezwa kisheria.

Sendiga anatumia fursa hiyo, kuwaelekeza wenyeviti wa halmashauri na wakurugenzi kuwabana watunza hazina wa halmashauri fedha zitengwe.

Mbunge wa Mbulu Mjini, Zacharia Isaay, anachangia hoja kuwa fedha hizo ni nyeti katika matumizi yake, huku Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, John Noya, anaiambia Nipashe kuwa suala la kutenga fedha hizo ni endelevu na uhamasishaji unaendelea.

**Inaendelea Uk. 13**

AFYA

# SIMULIZI YA BINADAMU ALIVYOTOKEA KWENYE UMBILE NA AFYA YA SOKWE

**Na Tuntule Swebe**

KIMSINGI, maisha ya binadamu yanaainishwa na asili kutoka kiumbe sokwe. Ni simulizi za kitafiti kwamba, binadamu walipitia hatua tofauti, hadi kukamilika umbile la sasa.

Mwanzo anatajwa, ametembea kwa miguu minne ikiwa ni chimbuko la miaka milioni tatu iliyopita, mnyama huyo akiweza kutengeneza zana kwa kutumia mawe.

Miaka ilivyoenda, kiumbe huyo akaenda kwenye hatua inayoitwa kitaalamu 'homo habilis', akitengeneza vifaa vyake vya kujihudumia.

Baada ya muda mrefu, ndio akaingia katika ngazi inayoitwa katika shoka, kisha baada ya kupita miaka mingi, akahamia katika umbile hilo la 'homosapien.'

Ishara anazotumia sokwe sasa, zinatajwa pia zipo kwa binadamu. Chanzo cha lugha za sasa, inarejewa ni ishara za sokwe, zikifanana kwa asilimia 95, na binadamu. Pia, nyani wakubwa wana ishara hizo, ingawa ufansi wa sokwe unatajwa kuwa juu zaidi.

Kingine katika ufafanuzi huo ni kwamba binadamu na sokwe, wote wanaelezwa kuhimili kula chakula cha moto, ikitoa ishara kwamba wanapika.

**JAMII ALIZOPITIA BINADAMU**


Kuna kinachoitwa Paleolithic; mazingira ya zama za mawe yenye mabadiliko lukuki, watu walihama na kuchangamana.

Watafiti wameweza kufukua masalia ya miili ya watu wa kale ipatayo 6,000 na ni michache kati yake imetoa ushahidi wa kijenetiki.

Historia ya mabadiliko ya binadamu, zinaonyesha jinsi watu wa kale walivyoishi katika maeneo mbalimbali.

**HATUA ZA MABADILIKO**

HOMO RUDOLFENSIS; Hao Homorudolfensis wakawa mfano bora kuwaelezea spishi kwa kuzingatia ushahidi wa ukomo wa masalia ya miili ya kale.





Marejeo ya uhusiano wa binadamu na sokwe, walikotokea kihistoria. **PICHA: MTANDAO.**

Ni historia inayomgusa binadamu na fuvu lake, akifahamika kama KNM-ER 1470 aliyeishi takriban miaka milioni 1.9 iliyopita, katika eneo lililoitwa Koobi Fora, ambalo sasa ndio Kenya.

Awali, fuvu hilo linasemekana ni la spishi wanaoitwa Homohabilis, ambaye ndiye kizazi cha zamani kabisa cha binadamu.

Mzizi wake unatajwa kuwa na meno mapana na mfupa mdogo sana wa juu ya macho na wana mienendo na tabia za kihistoria za binadamu.

HOMO ANTECESSOER; pango kubwa la Dolina ama The Gran Dolina Cave lililopo nchini Hispania, ni eneo kubwa la kiikolojia likiwa na ukubwa wa mita 20 na historia zaidi ya miaka nusu milioni imepita.

Aina hao ambao wameelezwa walikuwa na mchanganyiko wa maumbile ya kisasa na kizamani.

Eneo hilo limedumu kwa takriban miaka 780,000, likijumuisha masalia ya kikundi cha binadamu waliopewa jina la Homoantecessor.

Vilevile kuna Neanderthals na Denisovans, huku wengine wakifanana na Homosapiens.

Utafiti wa hivi karibuni kuhusu protini za kale zilizochukuliwa kutoka kwenye meno ya mojawapo ya mabaki ya 'spishi' aina ya Atapuerca, zimeonyesha kuwa H. antecessor ni 'dada' wa karibu mwenye uhusiano na mwanadamu wa sasa.

HOMOFLORESIENSIS; hao wanatajwa kuwa masalia yanayofahamika nchini Indonesia. Wanaakiolojia pia wanawaeleza 'spishi' hao wana utashi wa kibinadamu. Wote walikuwa na urefu zaidi kwa sentimita 90.

Binadamu hao wanatajwa kuwa na ubongo mdogo (takriban sentimita 400 za ujazo), waliwinda na zana zao zilifanana sana na zile zilizotengenezwa na aina ya Homoerectus, jamii iliyokuwa na ubongo mkubwa.

HOMOLUZONENSIS; ni mabaki ya binadamu wa kale yaliyogundulika karibuni walioishi kwenye kisiwa cha Luzon, nchini Ufilipino, miaka takriban 50,000 hadi 60,000 iliyopita.

Mwaka 2019, wanaanthropolojia walibaini kuwa mifupa yake ina tofauti na 'spishi' wengine kama H -erectus na H- floresiensis.

Kidole na mfupa wa mguu vya H-luzonensis, kinatajwa katika mwonekano kupinda kiasi.

HOMO LONGI; ni 'spishi' wanaotajwa ni binadamu wa kale wanatoka katika China, ambako fuvu lao kubwa zaidi lilipewa jina hivi karibuni la 'Dragon Man.'

Fuvu hilo kwa mara ya kwanza liligundulika miaka ya 1930 na karibuni likapatikana, hata likafanyiwa tathmini ya wanasayansi.

Inasemekana waliishi miaka takriban miaka 46,000 iliyopita. Hata hivyo, ukubwa wa ubongo unafananishwa kwa kulinganishwa na wa binadamu wa sasa.

Hata hivyo, katika majumuishi ya watafiti, kila aina moja ya mtu anapogundulika kuwa katika matawi ya familia ya binadamu, anakukumbusha maisha ya kale ya binadamu yanakanganya na bado kuna mengi ya kujifunza.

**MABADILIKO KIMAUMBILE**

Inatajwa hadi kufika umbile la mtu wa sasa, amepitia hatua kadhaa.

Chipanzii au Praimeti; inatajwa kuwa hatua ya mwanzo kabisa ya binadamu, miaka milioni 30 iliyopita, kabla ya kuzaliwa Kristo.

Hapo anatajwa kuwa na wasifu kama alitembea kwa miguu minne ya mbele ikitumika kukamatia na nyuma kusimamia.

Pia, wapo Australopithikasi walioishi miaka 12,000,000 Kabla ya Kristo; sifa zao zikiwa wakapata sura za kibinadamu, pia kutembea kwa miguu miwili.

Wengine ni Zinjathropasi aliyeishi miaka milioni tatu Kabla ya Kristo; ambao wakawa na sifa za kiwa wajuzi watengenezaji zana kwa kutumia mawe.

Wengine ni Homohabilisi; walioishi miaka laki tatu Kabla ya Kristo; hao wanatajwa waligundua utengenezaji vifaa, shoka lililotumia kuua wanyama, kuwachuna, kukata na kuchimbia shimo.

Utafiti unaotajwa na Chuo Kikuu cha St. Andrew, binadamu na sokwe Top of Form wanazungumza lugha moja, mathalan wote ni watumiaji ishara.

- **Kwa mujibu wa taarifa za kitafiti za vyuo vikuu.**

## SAMIA VITANI, BAJETI HALMASHAURI KWA KILA ALIYE TAABANI; AJIRA MAOFISA LISHE

Inatoka Uk. 12

**SURA YA KIMATAIFA**

Shirika la Afya Duniani (WHO), kwenye Ripoti ya Mwaka 2013, ilitoa mwongozo mpya wa tiba kwa watoto wenye utapiamlo uliokithiri kuwa tatizo kubwa kwa watoto mil. 20, wenye umri chini ya miaka mitano.

Ripoti hiyo inasema utapiamlo unajitokeza wakati mtoto hata kumhatarisha afya yake, mwili unakosa virutubisho muhimu, ikiwamo protini, chanzo kikuu ni kukosa chakula bora; mtoto anasinyaa na uzito wake uunapungua.

Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) katika Ripoti yake ya Februari 8 mwaka, huu imezitaja nchi tano bora za kulea watoto, kuwa ni; Estonia, Uhispania, Finland na Uholanzi, ikinena uchunguzi ulipofanywa mwaka 2020, ustawi wa watoto Japan unashika nafasi ya kwanza katika afya kwa ujumla, huku ikizingatia angalizo dhidi ya hatari za unene uliopitiliza.

UNICEF inaitaja nchi ya Estonia, watoto wanakabiliwa na utapiamlo mdogo, hewa na mazingira tulivu yasiyo na kelele ikilinganishwa na nchi yoyote tajiri, ikiwa na sera bora za uzazi kupewa siku 100 za mapumziko, watoto wanapishana kwa wastani miaka mitatu na likizo sahihi kwa wazazi.

Uhispania kunatajwa viwango vidogo au vya chini vya magonjwa ya watoto kutokana na utapiamlo wa hewa au maji; huku Finland kiwango cha vifo vya watoto wenye umri miaka mitano mpaka 14 ndiko chini sana duniani na kuna likizo inayojitosheza ya uzazi; Uholanzi kukiwapo ufanisi katika afya ya akili ya watoto na ujuzi.

**WADAU NAO WANENA**

Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Selina Msengi, anasema wanazalisha viini lishe vinavyokabili utapiamlo, akizitaja mbegu za lishe kwa majina; K1, Lishe H1 na Lishe H2, zinazotumiwa na wajawazito na wazee kuwaongezea lishe.

Mshauri wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC) Davis Gisuka, anasema ni vyema halmashauri zikaendelea kutenga Sh. 1000 kwa kila mtoto, kufanikisha juhudi za serikali kutoa elimu lishe.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) ya mwaka 2021/22-2025/26, inaeleza mtoto mmoja kati ya sita mwenye miezi 24 -35 wana udumavu mkali. Mikoa iliyoathirika kwa udumavu zaidi ya asilimia 40 ni Njombe asilimia 53.6, Rukwa 41.0, Iringa 47.1, Songwe 43.3, Kigoma 42.3 na Ruvuma 41.0.

PJT-MMMAM inasema nchini Tanzania kiwango cha utapiamlo sugu bado kipo juu na suala linalotia mashaka ikizingatiwa kuwa udumavu ni viashiria mojawapo kinachosababisha watoto kutofikia hatua timilifu za ukuaji.

*** Mwandishi wa makala anapatikana kwa mawasiliano: 0787598182.**

MAZINGIRA

## IKING'ARA UNDUGU WAKE NA WANAHABARI…

# Siku EWURA ilivyobanana na wahariri kupata majibu ya utitiri vituo vya mafuta

## •Yajivuna, usomaji mita za maji katika mageuzi

**Na Flora Wingia**



Moja ya vituo vya mafuta, vinavyotolewa ufafanuzi na EWURA. **PICHA: MTANDAO**

HIVI karibuni Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) lilifanya mkutano wake mkuu wa saba wa mwaka mjini Lindi. Mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. Wadau mbalimbali walipata fursa kutoa elimu mbalimbali kuhusiana na majukumu yake katika ujenzi wa taifa letu.

Miongoni mwa wadau hao ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) na kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Dk. James Andilile, mwasilisha mada alikuwa Meneja wa Mawasiliano Ewura, Titus Kaguo.

Wasilisho kwenye mkutano huo liliainisha namna vyombo vya habari nchini kupitia wasimamizi wao, vilivyochangia ufanisi katika utendaji kazi wa mamlaka hiyo nchini.

Kaguo anasema, Ewura kila baada ya miaka mitatu hufanya mapitio ya utendaji wake wa kazi. Pia, inafanya marejeo ya kumbukumbu zake kutaka kujua kwamba umma unavyopima kuhusu kazi inazozifanya.

Anataja mara ya mwisho ilifanyika mwaka 2019, likaonyesha undani wa kazi zao. Hata hivyo, pamoja na mfumo huo, ikabidi wafanye utafiti mwingine uliokamilika na kutoka mwezi Septemba mwaka huu.

Kwa mantiki hiyo, akasema vyombo vya habari kupitia wawakilishi wao Jukwaa la Wahariri, vimechangia kwa asilimia 100 kuleta matokeo hayo ambayo yametengenezewa ripoti inayoitwa 'Ewura the Customer Satisfaction Survey'. Kwa maana nyingine wateja wanavyoridhika juu ya utoaji wa huduma za Ewura.

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti, wanaoridhika na huduma za Ewura, wamefika asilimia 80.4 kutoka asilimia 67 mwaka 2019.

"Kwa hiyo, nataka kuwashirikisha kwamba mmeshiriki kuhakikisha Watanzania wanatuelewa kwa shughuli zetu tunazozifanya," anasema Kaguo.

### SURA YA NIDHAMU

Akitaja baadhi ya maeneo ambayo watu wanaielewa Ewura, mojawapo yanahusu nidhamu ya wafanyakazi wa Ewura.

Matokeo yameonyesha kwamba asilimia 92, wafanyakazi wa Ewura ni waaminifu asilimia 92.4 ilionyesha wafanyakazi wana bidii na asilimia 91.8 walionyesha wanatoa haki na asilimia 89.9 wafanyakazi Ewura wanaheshimika.

Akasema, ingekuwa vyombo vya habari vingekuwa havionyeshi jinsi Ewura inavyofanya vizuri, ina maana Watanzania wasingewajua katika mazingira haya.

"Kwa hiyo, tunatoa pongezi kwenu kwa kazi nzuri inayofanyika. Mapema mwaka huu, Ewura mwezi Februari ilishinda tuzo kama taasisi bora yenye uhusiano mzuri na vyombo vya habari. Na mimi nikashinda kama meneja uhusiano bora katika masuala ya nishati".

Kwa ripoti yake hiyo, Kaguo anasema asilimia 82.5 ya wafanyakazi wa Ewura walionekana wanaonyesha uhusiano mzuri na wateja wanaowahudumia.

Hata hivyo, yapo maeneo ambayo walisema yanahitaji maboresho, mfano kuwapo baadhi ya watendaji wanaweza kuwa na lugha siyo nzuri.

Kuhusu eneo la utoaji huduma za leseni, Kaguo anasema ilikuwa asilimia 84.7, leseni zinatolewa haraka na kwa usahihi. Pia, kukatajwa asilimia 73.3 ya wateja walielewa Ewura kupitia televisheni, radio, mitandao ya kijamii na magazeti.

"Ndio maana nakuja kwenu kwa kuwa ninyi mmefanya mchango kwa asilimia 73.3, Watanzania waielewe Ewura, japo zipo njia nyingine za kuelimisha juu ya mamlaka hii, kama vile semina, mikutano na kadhalika," anatamka.

Eneo lingine linatajwa ni mawasiliano, kukionyeshwa kwamba walioridhika na mfumo wa utoaji wa leseni unaoitwa 'lincensing order information' ni asilimia 89.2 kwamba Ewura inafanya vizuri.

Vilevile, kwenye mustakabali wa wa namna wanavyotoa elimu kwa umma, walipata asilimia 84.8. Kwa wale waliosema mawasiliano yao yako wastani (fair) ni asilimia 85.7 kutoka asilimia 50 mwaka 2019.

Kaguo akatoa salamu toka Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Dk. James Andilile, kwamba Watanzania kwa asilimia 84.4 wanaridhika na huduma zinazotolewa na Ewura.

### MASWALI

Pia, kabla ya maswali toka kwa wahariri, Kaguo akazungumzia eneo la maji na jinsi Ewura inaliwekea mkazo. Hapo kuna mfano mabadiliko ya sasa, kabla ya kulipa bili wateja wanaletewa ujumbe kuepuka hali ya kuibiana. Mita inaposomwa na watendaji wa mamlaka za maji, nayo ni lazima mwenye mita awepo.

Mita ikisomwa unajulishwa, unatolewa muda wa siku tatu kisha unaletewa bili na kama huridhiki unarudi ofisini inarekebishwa. Kama hakuna marekebisho ndani ya muda huo unaletewa bili ya kulipia.

Wahariri walipata wasaa kumuuliza Kaguo maswali kadhaa na kujibiwa. Kwamba kama baadhi ya bidhaa huuzwa bei moja mikoa yote, je, inashindikana vipi bei ya mafuta kuwa moja nchini.

Akajibu: Ni kweli kuna hoja, lakini tusichukulie uuzaji wa vinywaji tukafanya ni kwa taifa zima. Mtu anayekunywa soda Dar es Salaam,unaumia zaidi kuliko anayekunywa soda Songea, kwamba wewe ndiye unayemfidia aliye Songea.

Ila kwa kuwa soda ni Sh. 1,000 Dar es Salaam hadi Songea, unaona kama mko sawa. Lakini wa Dar es Salaam, pengine ilitakiwa iwe Shilingi 200.

Kwa kuwa ni mfanyabiashara binafsi anaweza kutoa ruzuku akahakikisha bei zinafanana. Ni sawa na gesi asilia. Mtungi wa gesi wa kilo 15 Dar es Salaam ni Sh.58,000/= hadi sh.60,000/=. Na ukifika Dodoma kilomita 460 bei ni takriban 58,000/= hadi 60,000/= , hapo ionekane bei ni sawa.

Kinachobadilisha bei za bidhaa kimsingi ni gharama za usafirishaji. Hivi sasa zinapangwa bei za mafuta katika bandari tatu, Mtwara, Dar na Tanga. Utaona mafuta yakitokea Mtwara bei inakuwa ndogo yakifika Lindi inakuwa kubwa kutokana na gharama za usafirishaji.

Ewura inafuatilia kuona mfumo utakaoleta bei moja Tanzania nzima. Aidha, utakuwapo mfuko ambao huko nyuma ulishakuwepo.

Ila wapo watu huvuruga, mtu anachukua risiti anaenda Kagera anagonga anasema nimefikisha mafuta Kagera wakati mafuta hayajafika huko. Tunafanya marejeo tuona tunakujaje na bei moja nchi nzima.

### VITUO VYA MAFUTA

Kuhusu ujenzi holela vituo vya mafuta maeneo hatarishi, Kaguo akasema, ujenzi wa vituo hivi kwanza anayesababisha viwepo siyo Ewura. Wahusika ni halmashauri za miji, mipango miji au jiji. Hao ndio wenye mpango mji kwamba hili eneo ni kanisa na kadhalika. Kwanini, Ewura inapokuja huwa na 'check list' kwamba mtu akifika kuomba kituo Ewura; kwanza awe na leseni ya biashara; pili ramani ya mpango miji; tatu leseni ya halmashauri; nne hatimiliki (title deed).

Anataja tatizo lipo kwenye halmashauri wanapobadilisha matumizi ya ardhi na kuweka vituo mahali pasipostahili. Hivyo, anayesababisha kituo kiwapo ni halmashauri ya mji, halmashauri ya mkoa au ya manispaa, anasisitiza Kaguo.

Kuhusu kuwa vituo vipo jirani hasa katika mikoa kama Dar es Salaam, tofauti na maeneo kama ya Lindi, anasema sheria iliyopo umbali wa kituo hadi kingine ni mita 200 ambazo ni sawa na viwanja viwili vya mpira. Ni suala chini ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kufanya mapitio upya kisheria.

Hata hivyo, vituo vipo kurahisisha wenye magari hasa wakati wa dharura. Amasema Ewura sasa wanaangalia pia usalama wa mazingira na mali za watu.

Swali, je, kituo hakina asili ya mlipuko? Hakitaathiri watu walio karibu? Ndio maana vingi vina ukuta mkubwa sana. Ifahamike kwamba chochote hatarishi Ewura haitoi leseni.



# Wajasiriamali 16,000 kuinuliwa kiuchumi

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

**Mradi mwingine utakaotekelezwa ni New Gunvor ambao lengo lake ni kusaidia wajasiriamali 9,750 asilimia 80 wakiwa ni wanawake ambao watatengeneza biashara 6,825 na ajira 11,700.**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Hand in Hand Eastern Africa Tanzania, limepanga kuwasaidia wajasiriamali 16,000 wa Mkoa wa Singida kuunda biashara 11,200 zitakazotengeneza ajira 17,388 ili kuwainua kiuchumi na kukuza mabadiliko ya kimfumo ya usawa wa kijinsia.

Meneja wa Shirika hilo tawi la Singida, Glory Temu, alisema hayo jana wakati wa kikao cha kutambulisha miradi itakayotekelezwa mkoani hapa kwa viongozi wa serikali na wananchi ambacho kilienda sanjari na ufunguzi rasmi wa ofisi za shirika.

Temu aliitaja miradi itakayotekelezwa na shirika hilo kuwa ni wa Inua ambao utasaidia wajasiriamali 6,250, asilimia 80 wakiwa ni wanawake na asilimia 20 wanaume ambao watаunda biashara 4,375 na kutengeneza ajira 5,688.

Alisema mradi huo utakaochukua miezi 41 kuutekeleza utatumia hatua nne za shirika ambazo ni uhamasishaji wa watu kujiunga kwenye vikundi, mafunzo ya biashara, kuwaunganisha wanavikundi kupata mikopo katika taasisi za kifedha na masoko.

Temu alisema matokeo yanayotarajiwa katika mradi huo ni kuongeza faida na uimara wa kibiashara kwa wanachama, kuinua kipato, kurasimisha shughuli za kuongeza thamani katika mradi na kusaidia vikundi kuunda asasi za kijamii (CBOs) na faida kutoka viwango vya kiuchumi.

Aliongeza kuwa mradi mwingine utakaotekelezwa ni New Gunvor ambao lengo lake ni kusaidia wajasiriamali 9,750 asilimia 80 wakiwa ni wanawake ambao watatengeneza biashara 6,825 na ajira 11,700.

Alisema mradi huo umepangwa kuchukua miezi 16 ambao pamoja na mambo mengine utasaidia kuondoa vikwazo vya kijinsia vinavyozuia uwezeshaji wanawake,mafunzo ya ziada ya jinsia ambayo yatashughulikia sheria zenye madhara ili kutetea usawa na ushirikishwaji wa wanawake.

Mtendaji Mkuu wa Shirika (CEO), Albert Wambungu, aliishukru serikali ya Mkoa wa Singida kwa kukubali kulipokea shirika hilo ili liweze kutekeleza miradi hiyo kwa manufaa ya wananchi na watashirikiana na serikali katika kila hatua ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Meneja wa nchi wa shirika hilo, Jane Sabuni, alisema Shirika la Hand in Hand Eastern Tanzania linatekeleza miradi mbalimbali katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma na Singida ambapo limewafikia wanachama wasiopungua 37,000, kuanzisha biashara 38,000 na kutengeneza ajira 39,000.

Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Utawala na Rasilimali Watu, Stephen Pancras, aliwasihi watendaji wa serikali kutokuwa kikwazo cha shirika hilo kufikia malengo yaliyokusudiwa na badala yake wahakikishe wanatoa ushirikiano.

## Waelimishwa kujikinga na magonjwa ya mlipuko

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Jiji la Dodoma wameshauriwa kujihadhari na mvua zinazoendelea kunyesha kwa kuweka mazingira yao katika hali ya usafi ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko ikiwemo kipindupindu.

Rai, hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa kitengo cha Usafi na Udhibiti wa taka ngumu jijini Dodoma, Dickson Kimaro, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dodoma.

Kimaro, aliwataka wakazi wa jiji hilo kuhakikisha kwenye maeneo yao muda wote yanakuwa katika hali ya usafi wa mazingira hasa kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha ili kujiepusha na milipuko ya magonjwa ya matumbo ikiwemo kipindupindu.

"Katika kipindi hiki cha mvua wakazi wote wa jiji la Dodoma ni muhimu zikachukuliwa tahadhari mbalimbali kwa kushirikiana kwa pamoja ili magonjwa hayo ambayo ni tishio tuweza kuepukana nayo na hii inawezekana tukiungana,"alisema

Hata hivyo, mkuu huyo wa kitengo cha usafi na mazingira pia amewataka wafanyakazi wake wanaojihusisha na uzoaji wa taka kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma wahakikishe wanatumia vitendea kazi walivyokabidhiwa.

Kimaro, pia aliwataka wauza matunda ndani ya masoko na mitaani kufuata sheria ikiwemo kuzingatia usafi wa mazingira kwenye biashara zao kwa ajili ya kujilinda na magonjwa yanayoweza kulipuka kwenye kipindi hiki cha mvua.

"Niwaombe wauza matunda masokoni na wale wanaotembeza mitaani wahakikishe sheria ya kiafya wanazingatia ili waepukane na magonjwa yanayoweze kulipuka na kuweka hatirini afya zao na hata kwa wateja wao pia"alisema.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, akizungumza wakati wa ufunguzi wa Siku 16 za Ukatili wa Kijinsia, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mkuu wa mkoa aagiza watoto wapewe mbinu kujikinga ukatili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewaasa wazazi na walezi kuwajengea watoto uwezo wa kujiamini na kujitambua ili kujilinda na vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ambavyo vimeshamili hivi sasa katika jamii.

Shenyamule, alisema hayo jana jijini hapa, wakati akihutubia kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Squre.

"Nitumie fursa ya kampeni hii ya siku 16 kuwakumbusha wazazi/walezi na jamii kuwajengea watoto wetu uwezo ili waweze kujitambua na kujilinda dhidi ya matukio ya ukatili kwani watoto wapo katika hatari zaidi ya kufanyiwa vitendo vya ukatili.

"Nitoe rai kwa watendaji katika ngazi mbalimbali kuhakikisha kunakuwa na mifumo ya utoaji wa msaada wa haraka pale inapobainika mtu amefanyiwa ukatili wa kijinsia ili manusura awezeshwe kupata huduma kwa haraka na kuepusha hatari zaidi," alisema Senyamule

Aidha, alitaja maeneo ya kutoa taarifa ikiwa mtu amefanyiwa ukatili kuwa ni pamoja na kituo cha huduma za afya, dawati la jinsia na watoto kwenye Jeshi la Polisi , Ustawi wa Jamii, serikali za mitaa na kijiji pamoja na mashirika ya huduma ya msaada wa sheria.

Alisema mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa watoto ni jukumu la kila mtu badala ya kuliacha kwa serikali au mashirika pekee yake.

Kadhalika, alisema kutokana na vitendo vya ukatili kushamili katika maeneo mengi nchini wazazi pamoja na Watanzania kwa ujumla kushirikiana na serikali kukomesha vitendo hivyo ambavyo vinachafua taswira ya nchi.

Maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia huanza kuadhimishwa kila ifikapo Novemba 25 kila mwaka yakiwa na kaulimbiu zenye ujumbe mbalimbali ambapo kwa mwaka huu ni "Nyumbani kwangu hakuna ukatili", na dhamira ya kampeni hii ni kuwahamasisha wanajamii kukemea ukatili kuanzia nyumbani.



# Utoaji taarifa ukatili kijinsia tatizo Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAWAKE katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, mkoani Njombe, wameelezwa madhara ya kutoripoti matukio ya ukatili wa kijinsia ikiwamo kipigo kutoka kwa wanaume zao kwa kuhofia ndoa kuvunjika.

Akizungumza na Nipashe, katika maadhimisho ya kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Herieth Magaji, alisema kitengo cha ustawi wa jamii kipo kwa ajili ya kusuluhisha migogoro na si kuvunja ndoa.

**Mtu anapotoa taarifa ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia itasaidia kuwaelimisha na kuwapatanisha ili kuweza kulea familia kuwa bora.**

Uzinduzi wa maadhimisho hayo ulifanyika chini ya uratibu wa Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo barani Afrika (WiLDAF), Mtandao wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (Mkuki) wa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

"Wakinamama wanaonewa, wanapingwa na wakati mwingine wanaingiziwa chupa sehemu za siri lakini hawasemi, wanasema kwamba mimi navumilia ndoa ndugu zangu watanicheka, majirani watanishangaa lakini pia watoto wataishi na nani," alisema Magaji.

Hata hivyo, Magaji alisema mtu anapotoa taarifa ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia itasaidia kuwaelimisha na kuwapatanisha ili kuweza kulea familia kuwa bora.

"Unapotoa taarifa sisi hatuna maana tunaachanisha ndoa yako au tunakwambia uondoke kwenye ndoa yako, bali tunasuluhisha mgogoro wako, tunasuluhisha kupitia kanuni na sheria ili uweze kuendelea kuishi kwa amani sio kwamba sisi tunatenganisha,"alisema.

Magaji alibainisha kuwa matukio mengi ya ukatili kwa wanandoa yanakuwa yamefanyika kwa muda mrefu bila ya kuripotiwa na matokeo yake yanasababisha madhara.

"Tunakesi kama hizi nyingi sana, ukija kwenye upelelezi wetu, uchunguzi wa kijamii wanajamii wanatumbia hao ni muda mrefu sana wanapigana, huyo mama ni muda mrefu anapingwa mpaka kuingiziwa chupa lakini hasemi ni msiri sana kisa anavumilia ndoa,"alisema Magaji.

Magaji alisema siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zimesaidia kupunguza kesi hasa za ubakaji kwa sababu ya hatua ambazo zinachukuliwa kupitia vyombo vya dola.

Kwa upande wa mkazi wa Njombe mjini, Farijika Gadau alisema wanawake wengi bado wanakabiliwa na uoga na kutokujiamini pamoja na vitisho kutoka kwa wanaume pindi anapomfanyia ukatili.

"Kwa sababu mwanaume mwingine anampiga mke wake na kumsisitiza kwamba ukienda kusema sehemu yeyote ntakuua kwa hiyo ule uoga unachangia mwanamke ashindwe kusema kwa kuogopa vitisho," alisema Gadau.

Gadua aliwataka wanawake kuacha kuwa wavumilivu katika kufanyiwa matendo ya kikatili na badala yake wabadilike kuokoa maisha yao.



Katibu wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC), Askofu Gelvas Nyaisonga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya jana, wakati akitoa taarifa ya baraza hilo, kuhusu maafa ya mafuriko yaliyotokea wilayani Hanang, mkoani Manyara, ambapo wametoa pole pamoja na misaada ya kibinadamu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wenye ulemavu waiomba serikali kuboresha miundombinu vyuoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wenye ulemavu wanaosoma katika vyuo vya ufundi stadi mkoani Mbeya wameiomba serikali kuboresha miundombinu ya vyuo hivyo ili iendane na mahitaji yao.

Walitoa maombi hayo kwenye Mahafali ya 23 ya Chuo cha Ufundi Stadi cha Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi yaliwakutanisha wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Mmoja wa wanafunzi hao, Joyce Sanga, mwenye ulemavu wa miguu alisema kwenye baadhi ya maeneo ya vyuo kuna majengo marefu ambayo siyo rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Alisema yeye anatumia kiti mwendo na hivyo anapokutana na maeneo yenye miundombinu isiyokuwa rafiki inakuwa vigumu kuingia darasani na kupata mafunzo kama ilivyo kwa wanafunzi wengine wasiokuwa na ulemavu.

Alisema chuo hicho cha Moraviani kimejaribu kuweka mazingira ambayo yanawawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kuingia na kujifunza lakini kwenye vyuo vingine hali haiku hivyo.

"Kama mlivyoona nimepatiwa vifaa ambavyo natakiwa nikafanyie kazi, lakini ukiangalia miundombinu ambayo ipo kwenye vyuo vingi huwa siyo rafiki kwa makundi yetu, hapa mimi nilikuwa naingia darasani kwa kutumia kiti changu kwa sababu hakuna majengo marefu," alisema Joyce.

Naye Rehema Mlawa ambaye, mwenye ulemavu wa miguu, alisema tatizo hilo linawafanya wanafunzi wengi wenye ulemavu kushindwa kufaulu masomo kwa sababu ya kushindwa kuendana na miundombinu iliyopo.

Alisema kwa sasa serikali imeweka sera ambazo zinawaruhusu watoto wote kupelekwa shule bila kujali hali ya viungo vyao lakini tatizo lililopo ni miundombinu kutokuwa rafiki.

Mkuu wa chuo hicho cha ufundi, Gadi Lwinga, alisema chuo hicho kinafanya juhudi mbalimbali za kutekeleza sera za nchi ikiwamo kusaidia watu wenye uhitaji maalum kwa kuhakikisha kunakuwepo miundombinu rafiki ya kuwawezesha kusoma kwa amani na utulivu.

Alisema chuo hicho kina utaratibu wa kudahili wanafunzi wenye ulemavu kila mwaka kwa lengo la kuwasaidia kupata fani wanazozihitaji kulingana na hali zao.

Kwa upande wake Askofu Mteule wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi, Robert Pangani alisema kanisa hilo litaendelea kuboresha miundombinu ili kuwasaidia wanafunzi wa makundi yote.

# Taasisi zenye malalamiko mengi Ikulu kuundiwa tume

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema taasisi za umma zitakazobainika kuwa na malalamiko mengi ya wananchi na watumishi wa umma yanayofikishwa Ikulu kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi, watendaji wake wataundiwa tume ili kama itabainika kuwa ni uzembe wachukuliwe hatua.

Hayo yalielezwa katika hotuba ya Katibu Mkuu Kiongozi, Prof. Moses Kusiluka iliyosomwa na Katibu wa Ikulu, Mluli Mahendeka alipokuwa anafungua mafunzo ya watumishi wanaosimamia nidhamu za watumishi wa umma kutoka katika mikoa sita ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema malalamiko hayo yatakuwa yanachunguzwa ili kubaini kama ni uzembe wa watumishi hao, ukosefu wa uadilifu ama kutozingatia sheria ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

"Malalamiko mengi yanayokwenda Ikulu kutoka kwa wananchi ama watumishi huwa ni uzembe, kukosekana kwa uadilifu ama uzembe, sasa tutakuwa tunayachunguza ili kubaini yanatokana na nini kabla ya kuchukua hatua," alisema Kusiluka.

Baadhi ya viongozi kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na viongozi wa tume ya utumishi wa walimu walisema mafunzo hayo ni muhimu kwao na yatawasaidia kuboresha utendaji kazi.



# Tanzania yataja mikakati kupambana na umaskini

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi, amesema Tanzania inaendelea na mikakati yake ya kupambana na umaskini ambayo imejikita zaidi katika kuzifikia huduma muhimu za kijamii kwa wananchi wake.

Alisema misaada inayotolewa na Benki ya Dunia (WB) kupitia mfuko wa IDA kwa kiasi kikubwa imesaidia kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya wananchi kiuchumi kwa upatikanaji kwa huduma muhimu za kijamii.

Dk.Mwinyi alisema hayo jana visiwani humo wakati akifungua Mkutano wa 20 wa Mapitio wa Miradi ya Maendeleo ya Ufadhili chini ya mfuko wa IDA ambapo mkutano huo uliwasharikisha zaidi ya wajumbe 300 ikiwemo magavana wa Benki kuu 75.

Dk Mwinyi alisema mpango wa kunusuru kaya masikini (TASAF) unaofadhiliwa na Benki ya dunia umeleta mabadiliko makubwa ya maisha ya wananchi waliopo vijijini na kumudu kuendesha familia zao.

Aidha aliitaja misaada inayotolewa na Benki ya dunia kupitia IDA ni pamoja na huduma zilizofikishwa hadi vijijini ikiwemo upatikanaji wa maji safi na salama ambao umewanufaisha zaidi ya wanawake milioni 4.7 waliopo vijijini.

Alisema huduma za nishati ya umeme ambazo zimefika hadi vijijini kwa kiasi kikubwa zimesaidia kuleta mabadiliko kwa wananchi ikiwemo kupunguza matumizi ya kuni kwa ajili ya kupikia na hivyo kunusuru na kulinda mazingira.

Aidha alisema kufikiwa kwa huduma hizo muhimu za kumechangia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo utalii na hivyo kukuza pato la taifa na wananchi na vijana kupata ajira.

Dk.Mwinyi aliitaka IDA kujikita zaidi katika kusaidia mabadiliko ya hali ya hewa ambayo athari zake ni kubwa huku zikihitajika fedha nyingi katika kupambana na matukio hayo.

Hata hivyo alisema Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha uongozi wake amejikita zaidi katika suala la kukabiliana na changamoto hiyo kuhakikisha mabadiliko makubwa yanafikiwa kwa wanawake waliopo vijijini katika matumizi ya nishati mbadala.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk.Mwigulu Nchemba, alipongeza WB kwa misaada iliyojikita katika maeneo muhimu ikiwamo kupambana na umasikini, miundombinu pamoja na sekta ya afya na elimu.

Alisema kupitia taasisi ya IDA Tanzania inaendelea kunufaika na misaada hiyo yenye lengo la ukuaji kwa uchumi pamoja na kujenga mazingira ya utawala bora.

Nchemba alihakikishia benki hiyo kuwa nchi inaitumia vizuri misaada yote inayotolewa na taasisi hiyo kwa lengo la kuleta mageuzi ya kiuchumi,maendeleo na utawala bora.

Rais wa WB Ajay Singh Banga, alisema amefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na serikali katika uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na ujenzi wa miundombinu ambao ndiyo utakaoharakisha maendeleo.

Aidha alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotumia vizuri fedha za misaada zinazotolewa na taasisi hiyo kwa kuzielekeza katika maeneo muhimu ya maendeleo.

Alisema Benki ya Dunia kupitia taasisi zake itaendelea kusaidia maendeleo wananchi kwa kuwa imeridhishwa na matumizi sahihi ya misaada inayotolewa hasa kwa wananchi wa vijijini.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Rais wa Benki ya Dunia, Ajay Banga, kabla ya kufungua Mkutano wa Kimataifa wa Tathmini ya Muda wakati wa mzunguko wa 20 wa Mapitio ya Benki ya Dunia (IDA20), Wilaya ya Magharibi "B" Unguja, jijini Zanzibar jana. Katikati ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum. **PICHA: IKULU**

## Utelekezwaji wa watoto bado janga

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema, wanawake wajane Zanzibar wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kutelekezwa na watoto baada ya ndoa kuvunjika.

Aliyasema hayo jana Ofisini kwake Kinazini Mjini Unguja, wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kupokea ugeni wa Jumuiya za Wajane Afrika ukiongozwa na Rais wake, Hope Nwakwesi.

Alisema Zanzibar ina wanawake wajane waliofiwa na waume zao na wale ambao ndoa zao zimevunjika baada ya kupewa talaka lakini changamoto kubwa ya utelekezwaji watoto inawakumbwa waliopewa talaka.

Alisema wizara yake kupitia idara ya ustawi wa jamii huwa inatatua changamoto hizo kwa kuziita pande zote ili kuhakikisha akina baba wanatoa huduma kwa watoto ingawa kwa baadhi yao ni vigumu kuwapata.

"Tunashukuru wengi wao hutoa ushirikiano, na kwa wale waliofiwa na waume zao tunapopata changamoto zao wizara huwasaidia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili watoto yatima wapate msaada,"alisema.

Aidha alisema wizara yake inapokea kesi ya wanawake kutelekezwa baada ya kuzaa watoto wenye ulemavu na ndoa zao zimevunjika kutokana na kuzaa watoto hao.

Alisema wanawake wenye watoto wenye uhitaji maalum huwa na changamoto kubwa ya makazi. Wengi wao hawana kipato hivyo hali inayosababisha kuwapo wimbi kubwa la watoto wa mitaani.

Aliishauri jamii kuacha tabia ya kuwatelekeza wanawake hao na badala yake kuwa nao karibu kwa hali na mali kwa kuwapatia misaada itakayowasaidia kupata mahali pa kujihifadhi.

Rais wa chama cha wajane Afrika, Hope Nwakwesi, alisema wamepigania mabadiliko ya sheria ya mirathi mpaka ngazi ya Umoja wa Mataifa lakini changamoto kubwa ni mila, dini na mambo mengine.

Alisema wanatarajia kufanya mkutano wa wajane Afrika mwaka 2024 ambao kwa mara ya kwanza utafanyika visiwani Zanzibar.

Aidha aliwataka viongozi wa nchi za Afrika kuwajengea uwezo wanawake wajane ili wapige hatua kubwa ya maendeleo inayotokana na nguvu za kiuchumi wawe na uwezo wa kukabiliana na changamoto nyingi zinazowakabili.

Alisema ni wakati sasa kuwapo na sera za kuwawezesha wanawake kiuchumi na kijamii hatua itakayosaidia kuondokana na changamoto ikiwemo hali ngumu ya maisha.

Alisema wanawake wakishiriki katika siasa na kuingia katika vyombo vya kutunga sheria kwa kiasi kikubwa sauti zao zitasikika na kuleta mabadiliko makubwa kiuchumi pamoja na kisera.

## Vifo vya uzazi bado changamoto Zanzibar

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa kati ya mwezi Januari hadi Octoba mwaka huu wazazi 61 wamefariki ndani ya siku 42 baada ya kujifungua katika hospitali za visiwani humo.

Hayo yalisemwa jana na Naibu waziri wa wizara hiyo Hassan Khamis Hafidh katika kikao cha baraza la wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Zawadi Amour.

Katika swali lake , Amour alitaka kujua Je, ni kipindi gani kitaalamu mwanamke huhesabiwa amefariki uzazi sambamba na watoto wanaozaliwa.

Naibu waziri huyo alisema kifo cha uzazi ni kifo ambacho kinatokea mara tu baada ya mama kupata ujauzito na ndani ya wiki sita baada ya kujifungua.

Aidha alisema ili kupunguza vifo hivyo wataalam wanashauri kinamama wahamasishwe kuhudhuria kliniki mapema mara tu baada ya kujigundua wana ujauzito.

Pia alisema wanapohudhuria kliniki ni jukumu la watoa huduma kuwaelimisha na kuwahamasisha wanajifungulia hospitali chini ya uangalizi wa wataalamu wa Afya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**Theresia Felix Mushi** anatangaza kupotelewa na Hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE245405** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/SON/MOM/2060/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATRICE BARNABAS TENGI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 198 CVV – TOYOTA PASSO**. Chassis namba **KGC100083384.** Engine namba **IKR0168631**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8661/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IBRAHIM INDUSTRIES LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 974 DUL - SCANIA. Chassis namba YS2G6X20005309878. Engine namba 006747720. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8171/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAVID PAUL NGILANGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 144 BSP - LANDROVER.** Chassis namba **SALLNABG12A220039.** Engine namba **JEVIC70262825K.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8171/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SINGIDA**
**LILILOPO SINGIDA**
**SHAURI LA MAOMBI MADOGO YA ARDHI NA. 65 YA 2023**
**SHABANI DAFFI........................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**ATHUMANI MANGU...........................MJIBU MAOMBI**
**KWA: ATHUMANI MANGU – POPOTE ULIPO TANZANIA**

### KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mwombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa Barazani ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo yanaweza kupatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe 8/12/2023 saa 2:00 asubuhi siku ya kutajwa kwa shauri hilo.
Unatakiwa uhudhurie mwenyewe au mwakilishi wako anaetambuliwa kisheria siku na saa tajwa hapo juu.
ANGALIA: Kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa na kusikilizwa upande mmoja wa mleta maombi tu na uamuzi kutolewa bila ya wewe au mwakilishi wako kuwepo.
HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya BARAZA hii leo tarehe 6 Mwezi wa Desemba, Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SINGIDA.

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**FARHANA NURU ALLY,** Anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE539765** Iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Tarehe 14/12/2022. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/11076/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA YA DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 321 YA MWAKA 2023**
**EMSON A. MNYAMILI...............................MLETA MAOMBI**
**VERSUS**
**OSCAL C. MNYASI..................................MJIBU MAOMBI**
**KWA: OSCAR C. MNYASI**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 14.12.2023 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 27 ya Mwezi wa NOVEMBA, 2023.

MWENYEKITI
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
DODOMA.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISRATE'S COURT OF MOROGORO**
**(EXTENDED JURISDICTION)**
**AT MOROGORO**
**EXT. JURIS. LAND APPEAL No.53 OF 2023**
**(Arising from High Court of Tanzania at Morogoro Land Appeal No. 113 of 2023, Original Land Application No.106 of 2021 of the District Land and Housing Tribunal for Morogoro at Morogoro)**
**AHMED SALUM MAZORA......................................APPELLANT**
**VERSUS**
**KONDO RAMADHANI NGOZI.............................1st RESPONDENT**
**MOHAMED ALLY MKUWE..............................2nd RESPONDENT**

**TO: KONDO RAMADHANI NGOZI**
**KIHONDA WARD**
**P. O. BOX 547**
**MOROGORO.**

**SUMMONS FOR PUBLICATION**

WHEREAS the Appellant have filed an Appeal against you, you hereby summoned to appear in this Court in person or by advocate duly instructed and able to answer all material questions relating to the Appeal or who shall be accompanied by some person able to answer all such questions on the 8th day of December, 2023 at 09:00 am in the forenoon before Hon. ASHA WAZIRI – PRM with Extended Jurisdiction to answer the case.
Take notice that, in default of your appearance on the day before mentioned, the case will be heard and determined in your absence.
Given under My Hand and Seal of the court this 1st day of December, 2023.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
MOROGORO

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
**0745 700 710.**
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Hali imekuwa mbaya Khan Younis, Hospitali zazidiwa miili ya waliokufa

**GAZA. Palestina**

VIKOSI vya Israel na wanamgambo wa Hamas, vinakabiliana katika mapambano makali katika kupambania kudhibiti mji wa Khan Younis ulioko kusini mwa Ukanda wa gaza.

Imeelezwa kwamba hali inazidi kuwa mbaya katika eneo hilo huku wanajeshi wa Israel wakionya wakazi wa mji huo kuhama ili kuepusha madhara.

Jeshi la Israel (IDF)lilisema linaendelea kufanya mashambulizi makali kwa sababu linaamini viongozi wa Hamas wamejificha katika mji huo.

Mji huo umekuwa kitovu cha mapigano makali kuanzia juzi na jeshi la Israel linaendelea kusisitiza kuondoka haraka kwa kufuata njia salama zilizotengwa.

IDF ilisema haitaruhusu raia kutumia barabara ya Salah al-Din ambayo inatumiwa kama njia ya uokoaji kutoka kaskazini mwa Gaza.

"Barabara hiyo ni uwanja wa vita na hatari sana kuifikia, Adraee alichapisha kwenye X.

Licha ya tahadhari hizo, kumekuwa na vifo vingi na kusababisha hospitali kuu kusini mwa Gaza kuzidiwa na miili ya watu.

Madaktari walisema wodi zimejaa na wagonjwa wamelala chini ya sakafu iliyotapakaa damu.

Kiwango hicho cha mapigano kinalazimisha watu 600,000 kuhamishwa kutoka kusini na kwenda Kaskazini mwa Gaza, hayo ni kulingana na Umoja wa Mataifa.

Jeshi la Israel liliushambulia kwa makombora mji huo wa Khan Younis ambao ni mkubwa zaidi kusini mwa Ukanda wa Gaza katika kile ilichokitaja kuwa ni mwendelezo wa kampeni yake ya kulitokomeza kundi la Hamas.

Taarifa ya IDF ilisema mapambano katika mji huo ndio makali zaidi tangu wanajeshi wake walipoingia Ukanda wa Gaza.

Jeshi hilo lilisema limelenga maeneo 250 kwa juzi pekee na limebaini maeneo kadhaa yanayotumika kuficha silaha, mahandaki na miundombinu mingine ya kijeshi.

Kundi la Hamas nalo lilisema kikosi chake cha wapiganaji cha al Qassam, kimewauwa na kuwajeruhi askari 8 na kuharibu magari 24 ya jeshi la Israel.

Maafisa wa Afya wa Ukanda wa Gaza walisema mashambulizi ya Israel yamesababisha vifo vya raia wengi hasa katika shambulizi lililolenga nyumba za makazi kwenye kitongoji cha Der al-Balah kilichopo kaskazini mwa mji wa Khan Younis.

Mkuu wa hospitali ya A.-Aqsa Eyad Al-Jabri alisema watu 45 waliuwawa.

Tangu kuvunjika kwa mkataba wa kusitisha mapigano Ijumaa iliyopita, jeshi la Israel limekuwa likitoa ramani ambayo inataka watu kutumia wakati wakihama kwenda maeneo salama.

Wakazi wa Gaza walisema hawana tena sehemu salama ya kujinusuru na makombora ya anga na ardhini ya vikosi vya Israel.

Kwenye hospitali kuu ya mji wa Khan Younis ya Nasser, majeruhi wanapelekwa kwa kutumia magari ya wagonjwa, malori na wengine wanabebwa na punda.

Mwandishi wa shirika la habari la Reuters alisema ndani ya wodi ya wagonjwa kila eneo limetapakaa damu na hakuna sehemu ya kukanyaga kutokana na idadi kubwa ya majeruhi.

Umoja wa mataifa umeionya Israel kutokana na majeshi yake kuyalenga maeneo ya makazi na kutishia Maisha ya watu wengi.

Inakadiriwa watu miloni 1.8 wanaoishi kwenye ukanda huo wamehama makazi yao, ikiwa ni asilimia 80 ya raia wote wa eneo hilo.

Wakati huo huo Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu ameashiria kwa mara ya kwanza kuwa jeshi la nchi hiyo litachukua jukumu la kulinda ndani ya Ukanda wa Gaza hata baada kumalizika.

Kiongozi huyo alisema vikosi vya Israel vitabidi vidhibiti kiasi fulani ya kiusalama kwenye Ukanda huo ili kuzuia kutokea tena mashambulizi dhidi ya Israel.

**DW**



Raia wa mji wa Khan Younis wakiangalia jengo ambalo lilishambuliwa na vikosi vya Israel jana. **PICHA: REUTERS**

# Wagombea DRC waonywa lugha za chuki, ukabila

**KINSHASA, DRC**

WIKI mbili baada ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi mkuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) taasisi mbalimbali za kimataifa zinazofuatilia uchaguzi huo zimewaonya wagombea kuacha kutumia lugha inayochochea chuki za kikabila.

Taasisi yenye waangalizi wa kimataifa na kitaifa , Symocel, ilielezea wasiwasi wake kufuatia kile inachokiona kuenea kwa kampeni za chuki dhidi ya baadhi ya wagombea, hali ambayo inaweza kuzusha vurugu kati ya makabila.

Katika kipindi cha kampeni kumeshuhudiwa baadhi ya wagombea urais wakitoa hotuba katika maeneo tofauti ya nchi, wakihoji kuhusu uraia wa watu wengine, na hata kuwataja wengine kuwa wagombea wa wageni.

Vyombo vya habari vilisema ghasia ziliripotiwa, katika majimbo ya Haut-Katanga, Bandundu, Kindu na Kinshasa eneo la Limeté zilitokana na maneno ya chuki za kikabila.

Symocel ilitoa wito kwa wanasiasa wa DRC kuvumiliana na kufanya kampeni zao kistaarabu, ili kudumisha amani nchini humo.

**RFI**

**Katika kipindi cha kampeni kumeshuhudiwa baadhi ya wagombea urais wakitoa hotuba katika maeneo tofauti ya nchi, wakihoji kuhusu uraia wa watu wengine, na hata kuwataja wengine kuwa wagombea wa wageni.**

# Rais Jong Un atoa machozi hadharani

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

RAIS wa Korea Kaskazini Kim Jong/kim-jong-un ametoa machozi hadharani wakati akiwasihi wanawake wa nchi hiyo waongeze watoto kutokana na taifa hilo kukabiliwa na upungufu wa watu.

Katika hutuba yake iliyojaa hisia alisema wanawake hao wazae watoto zaidi na kuwalea kama wajamaa.

"Kukomesha kupungua kwa idadi ya watoto wanaozaliwa na kutoa matunzo bora ya watoto na elimu ni mambo yetu wote ambayo tunapaswa kutatua pamoja na mama zetu," alisema kiongozi huyo huku akitokwa machozi na kujipangusa kwa leso yake nyeupe.

Kiongozi huyo alikuwa katika kongamano la tano la kitaifa la Wanawake lililofanyika mjini Pyongyang.

"Kuzuia kushuka kwa viwango vya kuzaliwa na malezi bora ya watoto ni majukumu yetu katika utunzaji wa familia tunayohitaji kushughulikia tunapofanya kazi na akina mama," alisema Kim Jong Un.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu linakadiria kuwa kufikia mwaka wa 2023, wastani wa idadi ya watoto wanaozaliwa na mwanamke nchini Korea Kaskazini, ilifikia 1.8, kiwango ambacho kimeshuka kwa kasi kwa kiwango hicho katika miongo ya hivi karibuni.

**BBC**

# MASHABIKI KUISHUHUDIA TAIFA STARS AFCON KI-VIP

**Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa soka nchini wamepewa fursa ya kwenda 'kibabe' katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2024), wakiishuhudia mubashara Timu ya Taifa (Taifa Stars) ikipeperusha bendera katika fainali hizo, imeelezwa.

Fainali za AFCON zinatarajia kufanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwakani huko Ivory Coast.

Akizindua kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, Rugambwa Juvenalius, Ofisa Habari wa Betika Tanzania, alisema kampuni yao imejipanga kuwapa fursa mashabiki wa soka kwenda kushuhudia fainali hizo kwa gharama za Betika.

Alisema mashabiki hao ni wale watakaoibuka washindi katika promosheni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP inayoendeshwa na Tigopesa kwa kushirikiana na Betika iliyozinduliwa jijini, Dar es Salaam jana.

"Mabingwa sita wa kampeni hii watagharamiwa usafiri na malazi kwenda kushuhudia fainali hizo nchini Ivory Coast," alisema na kuongeza," alisema.

Meneja Biashara wa Tigopesa, Fabian Feliciane, alisema huo ni mwendelezo wao wa kusapoti soka na kutoa fursa kwa mashabiki ambao ni wachezaji namba 12 uwanjani kuishuhudia Stars katika fainali hizo mubashara.

"Ni rahisi kupata nafasi hii, unachotakiwa ni kuweka pesa kwenye Tigopesa yako na kubeti na Betika," alisema na kuongeza.

"Pia kutakuwa na zawadi nyingine za kila siku na kila wiki za fedha taslimu na luninga na kumaliziwa na droo kubwa ya washindi watakaokwenda AFCON ifikapo Januari,".

Stars itashiriki AfCON 2024 kwa mara ya tatu baada ya kukata tiketi ya kwanza mwaka 1980 fainali zikichezwa Nigeria na mwaka 2019 huko Misri.

Stars ilifuzu baada ya kupata sare ya bila kufungana na wenyeji Algeria katika mchezo wa mwisho wa Kundi F na kumaliza hatua hiyo ikiwa na pointi nane, nyuma ya vinara, Algeria waliofikisha pointi 16.




Wafanyakazi wa Kampuni ya Betika Tanzania wakionyesha mfano wa tiketi katika uzinduzi wa kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP itakayowapa fursa mashabiki wa soka nchini kwenda kushuhudia mubashara fainali za AFCON 2024 zitakazofanyika Ivory Coast. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kili Marathon 2024 watoa neno

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDAAJI wa Mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager 2024 wamewakumbusha washiriki zimebaki siku chache kufurahia punguzo la awali ambapo watalipa chini ya kiingilio halisi kama wakijisajili kabla ya Desemba 14, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na waandaji inasema dirisha la awali limefunguliwa na washiriki wanatakiwa kutumia fursa hii kujisajili kwa wingi na kuepuka msongamano dakika za mwisho.

"Dirisha la awali la usajili lilianza Oktoba 16 na litaendelea hadi usiku wa manane wa Desemba 14, mwaka huu. Baada ya hapo kiingilio kitapanda katika makundi yote na kwa mataifa yote kutoka Desemba 15 hadi Februari 5, mwakani au hadi tiketi zitakapomalizika kutokana na nafasi finyu zilizopo," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Waandaji walisema washiriki wanaweza kujisajili kupitia Tigopesa kwa kupiga *150*01#, kisha bonyeza 5 LKS, kisha bonyeza 5 (tiketi) na fuata maelekezo kujisajili au kwa njia ya tovuti rasmi www.kilimanjaromarathon.com.

Bia ya Kilimanjaro ndio mdhamini mkuu wa mbio za masafa marefu na imeshika nafasi hiyo tangu kuanzishwa kwa mbio hizo miaka 22 iliyopita.

Wadhamini wengine ni Tigo (kilomita 21) Gee Soseji (kilomita tano), wadhamini wa meza za maji (Simba Cement, Kilimanjaro Water na TPC Sugar) wakati wabia rasmi ni KiliMedair, Garda World Security, CMC Automobiles, Hoteli za Sal Salinero, Kibo Palace na Keys Hotel.

Mbio za Kili Marathon zitafanyika Februari 25, mwakani na zimeandaliwa na Kampuni ya Kilimanjaro Marathon na kuratibiwa na Executive Solutions limited.

## Pamba yarejesha uhai Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Pamba FC imepanda hadi katika nafasi ya pili ya katika msimamo wa Ligi ya Championship baada ya kuitandika Fountain Gate Talents mabao 2-1 katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro juzi.

FGA Talents ilianza kupata bao dakika ya 16 lililofungwa na Andrew Chamungu, lakini dakika sita baadaye, Daniel Joram aliisawazisha Pamba na dakika ya 69 wakazi hao wa Mwanza walipata goli la ushindi ambalo wenye walijifunga kupitia, Anack Mtambi.

Ushindi huo wa juzi katika mechi ya raundi ya 13 ya ligi hiyo ambayo itatoa mbili timu zitakazopanda daraja na kutinga katika Ligi Kuu Tanzania Bara moja kwa moja na ya tatu kucheza mechi ya mchujo, umeifanya timu hiyo kufikisha pointi 27 nyuma ya vinara, KenGold ya Mbeya yenye pointi 29.

Pamba FC imekwea hadi nafasi ya pili katika hali ambayo haikutegemewa, ikinufaika zaidi na kipigo cha mabao 2-0 ilichokipata TMA ya Arusha dhidi ya KenGold, lakini Mbeya Kwanza nayo ilipoteza mechi yake kwa kufungwa magoli 2-1 dhidi ya Pan African, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

## Choki Junior rasmi bosi Extra Bongo

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Extra Bongo ambayo ilifufuliwa hivi karibuni baada ya kufa zaidi ya miaka nane iliyopita, kwa sasa ipo chini ya bosi mpya, Choki Junior.

Akizungumza katika uzinduzi wa bendi hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, mwimbaji mkongwe wa bendi hiyo, Ally Choki, alisema kwa sasa yeye anabaki kuwa mwenyekiti wa bendi na amempa mtoto wake jukumu la ukurugenzi.

"Mimi sio mkurugenzi tena kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, nimebaki kuwa mwenyekiti, Choki Junior ndiye Mkurugenzi mpya wa Extra Bongo ambayo pia inaitwa Baba Lao," alisema Choki.

Mwimbaji huyo alitaja sababu za kumpa cheo hicho mwanaye ambaye pia ni mwimbaji ni kutaka ajifunze jinsi ya kuongoza bendi na kupata uzoefu kama wake (Choki) ili kuiwezesha kusonga mbele.

"Kazi yangu itakuwa ni kumsimamia na kumwelekeza njia ya kupita katika uongozi wake, ili hata kama sipo, bendi ya Extra Bongo Baba Lao iendelee kutoa burudani kama kawaida," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PALHINHA AGOMBEWA ULAYA

BAYERN Munich itakabiliana na ushindani kutoka kwa klabu mbili za Ligi Kuu England wakati wa kumnunua kiungo wa Fulham na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Palhinha, mwenye umri wa miaka 28 ifikapo Januari (**Telegraph).**

### JOTA KUMFUATA ANGE

WINGA wa Al-Ittihad Jota mwenye umri wa miaka 24 anataka kuungana na kocha wake wa zamani wa Celtic, Ange Postecoglou katika klabu ya Tottenham Hotspur. **(Sun)**

### GUIRASSY AINGIA SOKONI

KLABU ya Manchester United pia imeungana na Newcastle, Roma na AC Milan katika kinyang'anyiro cha kumnunua mshambuliaji wa Stuttgart na Timu ya Taifa ya Guinea, Serhou Guirassy, mwenye umri wa miaka 27. **(Foot Mercato)**

### TOMIYASU ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inajadiliana na mlinzi wa Timu ya Taifa ya Japan, Takehiro Tomiyasu kuhusu mkataba mpya huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ukitarajiwa kukamilika 2025. **(Athletic)**

### DRAGUSIN ATAKWA UNITED

KLABU ya Manchester United inajadiliana kuhusu usajili wa beki wa Timu ya Taifa ya Romania na Genoa, Radu Dragusin, mwenye umri wa miaka 21. **(Prosport)**

### JUVENTUS KUIKAMUA SPURS

BEI ya winga wa Juventus, Samuel Iling-Junior, mwenye umri wa miaka 20 sasa imetajwa kuwa ni euro milioni 18 kutoka euro milioni 20, na Tottenham wanavutiwa na mchezaji huyo**. (Calciomercato)**

### GUEHI KUBAKIA PALACE

MARC Guehi anataka kusalia Crystal Palace hadi usajili wa majira ya joto ili kuongeza nafasi yake ya kujiunga na kikosi cha England kwa ajili ya Euro 2024. Beki huyo mwenye umri wa miaka 23 ananyatiwa na Manchester United pamoja na Newcastle United. **(90 min)**

### NYOTA AICHAGUA MADRID

MCHEZAJI Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 22 anayekipiga Napoli anayesakwa na Chelsea huenda akavutiwa zaidi kuhamia Real Madrid, kwa mujibu wa babake yake**. (Geo Team, via Express)**

### CITY KUMTOSA PAQUETA

KLABU ya Manchester City iko tayari kuachana na mpango wa kumnunua kiungo wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta, mwenye umri wa miaka 26, ikiwa suluhu kuhusu uchunguzi wa kamari dhidi ya mchezaji huyo hautakuwa umepatikana. **(Mail)**


### SUAREZ AMFUATA MESSI

MSHAMBULIAJI wa Gremio na Uruguay, Luis Suarez, mwenye umri wa miaka 36, anatazamiwa kuungana tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi, katika klabu ya Inter Miami kwa mkataba wa mwaka mmoja. **(Miami Herald)**

### LOPETEGUI ATAJWA UNITED

KOCHA wa zamani wa Wolves, Julen Lopetegui, alikataa mkataba wa pauni milioni 15.4 kwa msimu kutoka Al-Ittihad ya Saudi Arabia na kuamua kubakia katika Ligi Kuu England, huku Manchester United ikiwa miongoni mwa klabu zinazohusishwa kutaka kumwajiri Mhispania huyo. **(AS)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA KUIKOSA VILLA JUMAMOSI

Kocha huyo atakuwa anatumikia adhabu ya kadi tatu za njano ambazo...

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, hatakuwa kwenye benchi katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Aston Villa baada ya kupewa kadi ya njano ya tatu msimu huu kwa kusherehekea bao la ushindi la Declan Rice la dakika ya 97 dhidi ya Luton, juzi.

Mhispania huyo aliupita mstari wake na kuingia uwanjani kusherehekea bao hilo na benchi lake la ufundi.

Arteta alionyeshwa kadi ya njano na mwamuzi, Samuel Barrott, kumaanisha sasa hatakuwa kwenye benchi katika mchezo wa keshokutwa kwenye Uwanja wa Villa Park, kwa sababu kadi tatu za njano ni sawa na kufungiwa mchezo mmoja.

Alipoulizwa kama inafaa, Arteta alijibu: "Ndio, singeweza kukaa kwenye kiti changu, kwa bahati mbaya. Kwa hiyo niliondoka hapo, sikuwa na ufahamu hata kidogo.

"Zilikuwa hisia tu. Kwa hiyo ikiwa hiyo ni ya njano ni sawa tu."

Arsenal walianza kufunga wakati Gabriel Martinelli alipopachika wavuni baada ya kutengenezewa krosi ya chini chini kutoka kwa Bukayo Saka, ingawa Luton alirudisha haraka wakati Gabriel Osho alipofunga kwa kichwa kutoka upande wa kona na kufanya 1-1.

Kikosi cha Arteta kilipata bao la kuongoza kabla ya mapumziko, Gabriel Jesus akipiga kichwa kumpita Thomas Kaminski kwenye lango la baada ya mchezo mzuri wa kiungo Saka na Ben White upande wa kulia, lakini wakabanwa tena muda mfupi baada ya kipindi cha pili na Elijah Adebayo aliyetoka benchi.

Bao la Barkley akafunga bao kwa kazi nzuri ya Raya, lakini uongozi huo ulifutika ndani ya dakika chache wakati Kai Havertz alipofunga bao lake la tatu katika mechi nne na kufanya matokeo kuwa 3-3.

Wakati mchezo ukionekana kumalizika kwa sare Rice alifunga bao dakika za jioni na kuipa ushindi Arsenal.

Arteta alisema: "Nilifurahia sana, hasa mwisho.

"Ni jambo la kushangaza kuhusu soka, hisia na nyakati mnazoishi pamoja. Ulikuwa ni usiku wa kipekee.

"Tunamshukuru Luton kwa mazingira ya ajabu waliyounda na jinsi walivyocheza. Walifanya maisha kuwa magumu sana kwetu. Lakini tulipata njia ya kushinda. Ustahimilivu na tabia na ubora ulionyesha.

"Tunacheza kila baada ya siku tatu, na lazima tushinde kila mchezo, mahitaji yapo. Ni njia (wachezaji) wanavyoifanya, ni kiasi gani wanachotaka."

# MESSI MWANAMICHEZO BORA WA TIMES 2023




**NEW YORK, Marekani**

LIONEL Messi amechaguliwa kuwa Mwanamichezo Bora wa Jarida la Time kwa mwaka 2023 baada ya kuhamia Marekani, alikojiunga na klabu ya Inter Miami.

Messi anajiunga na wachezaji kama Simone Biles, Michael Phelps, LeBron James na Timu ya Taifa ya Wanawake ya Marekani kushinda tuzo hiyo.

Mshambuliaji wa New York Yankees, Aaron Judge, alishinda tuzo hiyo mnamo mwaka 2022.

Messi alicheza mechi yake ya kwanza kwa timu hiyo yenye maskani yake Florida Julai na alitangazwa kuwasili kwake kwa kufunga mkwaju wa faulo katika dakika za mwisho na kuipa timu yake ushindi wa 2-1.

Tangu wakati huo amekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Ligi Kuu Marekani.

Wakiwa na usajili wao wa nyota kwenye ubao, Inter Miami walishinda Kombe la Ligi, taji lao la kwanza kuu, wakiwashinda Nashville kwenye fainali ambayo Messi alifunga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alifunga mabao 11 katika michezo 14 katika mashindano yote kabla ya kumaliza msimu.

Mnamo Oktoba, mwaka huu alitwaa Ballon d'or baada ya nane baada ya kuiongoza Argentina kushinda Kombe la Dunia, Qatar mnamo mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alishindwa kurejea Barcelona na akakataa kuhamia Saudia kabla ya kusaini na Inter Miami kwa mkataba ulioripotiwa kuwa wa thamani ya dola milioni 20 kwa mwaka, na kile kinachoripotiwa ni dau la umiliki wenzake katika klabu hiyo atakapostaafu.

# Suarez kumfuata Messi Marekani

**MIAMI, Marekani**

LUIS Suarez anatazamiwa kujiunga na Inter Miami wiki ijayo huku vyanzo vya habari vikithibitisha makubaliano kati ya pande hizo mbili yamekamilika.

Kama 90min mchezaji huyo kila wakati alitaka kuungana na wachezaji wenzake wa zamani Lionel Messi na Sergio Busquets huko Florida.

Ingawa Suarez alikuwa na nia ya kujiunga na Herons msimu wa joto, alisalia chini ya mkataba na Gremio ya Brazil. Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 na Gremio utaendelea hadi 2024, lakini una kifungu cha kutolewa ambacho yeye na Miami wameanzisha.

Tetesi za kukaribia kuwasili kwake ziliibuka wiki iliyopita baada ya Kocha Mkuu Renato Gaucho kufichua kuwa Suarez alicheza mchezo wake wa mwisho akiwa na timu hiyo.

Mchezaji huyo kisha aliingia kwenye mtandao wa kijamii na kuandika kwaheri: "Mimi na familia yangu tunataka kumshukuru kila mtu kwa upendo na kile tulichoishi kwenye Uwanja wa Arena Do Gremio. Ilikuwa siku ya ajabu, isiyosahaulika ambayo tutaiweka mioyoni mwetu milele."

Vyanzo sasa vimethibitisha kuondoka kwake kutoka Gremio kutafuatiwa na kuhamia Inter Miami.

Jordi Alba, Busquets, Messi na Suarez walicheza pamoja mara ya mwisho mwaka 2020 wakiwa Barcelona, kabla ya Suarez kwenda Atletico Madrid.

Wachezaji wanne walivunja rekodi za La Liga, na kubeba mataji 10 yakiwamo mataji matatu ya ligi na matatu ya Copa del Rey.

Sasa, wanne hao wataungana tena katika Ligi Kuu Marekani kujaribu kushinda kombe la kwanza kabisa la ligi ya timu hiyo.

# Guardiola : Tutabeba tena ubingwa wa EPL

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola alisema uchezaji wa Manchester City kwenye sare dhidi ya Liverpool na Tottenham Hotspur umemshawishi timu yake itashinda tena taji la Ligi Kuu England msimu huu.

City wametoka sare michezo mitatu iliyopita dhidi ya Chelsea, Liverpool na Tottenham na kuporomoka hadi nafasi ya tatu katika msimamo.

Hata hivyo, kabla ya safari ya kucheza na Aston Villa jana Jumatano, Guardiola alisema ana uhakika watashinda taji la nne mfululizo.

"Hisia zangu leo tutashinda Ligi Kuu," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Ikiwa tutacheza kwa viwango tulivyoonyesha dhidi ya Liverpool na Tottenham, tutashinda tena.

"Watu hawaamini tayari baada ya sare tatu lakini tunahisi tutafanya tena, tukijua kwamba ni. si rahisi kwa sababu hakuna timu iliyofanya hivyo bado ilishinda nne mfululizo.

"Ugumu upo na ulikuwa msimu uliopita lakini ukiniuliza leo ninahisi nini, tutafanya tena."



HABARI MICHEZO

# SIMBA: TUTAWASHANGAZA WYDAD NYUMBANI KWAO

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Simba wameahidi kucheza kwa nguvu ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca itakayochezwa keshokutwa jijini Marrakech, Morocco.

Kikosi hicho cha Wekundu wa Msimbazi kiliwasili salama kikiwa chini ya Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha na kuanza mazoezi kuelekea mchezo huo wa tatu wa hatua ya makundi.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mara baada ya kutua Marrakech, Benchikha alihitaji kuanza mara moja mazoezi ili kuhakikisha nyota wake wanaimarika na kuwa tayari kwa mapambano.

"Kocha alihitaji siku tatu za mazoezi, siku ya Jumatano, Alhamisi (leo) tutaendelea na Ijumaa pia, kabla ya kucheza mechi yetu Jumamosi kwa ajili ya kupigania kuondoka na pointi tatu dhidi ya Wydad na hii yote amezingatia zaidi katika utimamu wa mwili.

Amesema (kocha), kikosi chetu kiufundi kikosi vizuri, lakini tatizo ni utimamu na kwa sababu hiyo ameomba siku hizo ili kukiweka sawa," alisema Ahmed.

Nahodha msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema wachezaji wapo tayari kwa mchezo huo na wanatarajia kusaka ushindi wa ugenini licha ya kufahamu wanakutana na timu kubwa.

"Tutapambana kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, ila najua utakuwa mchezo mgumu kwa sababu wenzetu hawajapata matokeo yoyote ya ushindi mpaka sasa lakini sisi tuna pointi mbili katika kundi, tunafahamu ugumu wa Wydad, ugumu wa kundi letu, lakini tunafahamu umuhimu wa kuzipata pointi tatu," alisema beki huyo wa kushoto.

Winga wa timu hiyo, Luis Miquissone, alisema kikosi kiko kamili kwa ajili ya kupambana ili kuwarudishia furaha wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

"Nafikiri tupo tayari kwa mechi hii, tutapigana, tupo tayari kwa mapambano, najua ni ngumu, Wydad ni timu kubwa na nzuri, lakini tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kwa ajili ya wanachama na mashabiki wetu na nchi kwa ujumla, watusapoti, tutawafanya wawe na furaha na hii ndiyo nafasi ambayo endapo tukishinda tutajiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye kundi letu," alisema nyota huyo raia wa Msumbiji.

Simba inashika nafasi ya tatu katika Kundi B ikiwa na pointi mbili wakati Wydad Casablanca ambayo haina pointi hata



Wachezaji wa mpira wa miguu kutoka Kituo cha Lumbuko wakifanya mazoezi ili kukuza vipaji vyao kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mgunda atajwa kutua Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja baada ya kupata suluhu kwenye uwanja wake wa nyumbani, Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya, uongozi wa Ihefu SC umeachana na kocha wake raia wa Uganda, Moses Basena, imefahamika.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema tayari viongozi wa klabu hiyo wameanza kufanya mazungumzo na kocha mkongwe, Juma Mgunda, ili kuchukua nafasi ya Basena.

"Uongozi wa timu yetu (Ihefu), umefikia makubaliano ya pande mbili ya kuvunja mkataba na aliyekuwa kocha wetu Mganda, Moses Basena.

Tunamshukuru Basena kwa wakati wote aliokuwa nasi ndani ya timu kama Kocha Mkuu na klabu inamtakia kila la kheri katika maisha yake mapya ya soka," iliandika taarifa hiyo.

Basena anaweka rekodi ya kuwa mmoja wa makocha walioifundisha timu hiyo kwa muda mfupi ambapo alianza kazi hiyo katikati ya mwezi uliopita akichukua nafasi ya Zuberi Katwila, na hajadumu hata mwezi mmoja.

Kocha mwingine ambaye hakudumu katika timu ni Mjerumani, Ernst Middendorp, aliyekuwa anaifundisha Singida Fountain Gate ya mkoani Singida.

Basena aliyeiongoza timu hiyo kwenye michezo saba ni hajashinda hata mchezo mmoja, akipoteza mitatu na kuvuna sare mara nne.

Ihefu haijashinda mechi yoyote tangu ilipowafunga mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga mabao 2-1, mechi iliyochezwa Oktoba 4, mwaka huu.

## Gamondi aongeza dozi Yanga SC

INATOKA UK. 24

zilizosalia.

"Tunafahamu haitakuwa mechi rahisi, kwa sababu Kocha Gamondi anaendelea kufanyia kazi mapungufu ya kikosi kufuatia makosa tuliyofanya katika mechi zilizopita ikiwamo kufanyia kazi ubora wa Medeama, tunajua wapinzani wetu kila mechi wamefanikiwa kufunga," alisema meneja huyo.

Daktari wa Yanga, Mosses Etutu, alisema wachezaji walioko Ghana wote wako vizuri na wanaendelea vyema na mazoezi kuelekea mechi hiyo na kila mmoja yuko tayari kutumikia majukumu yake.

Hata hivyo Etutu alisema kiungo, Jonas Mkude, alipata shida baada ya kula chakula lakini changamoto hiyo ilifanyia kazi na hali yake imerejea vyema huku Joyce Lomalisa, amebainika kupata jeraha dogo na atakuwa nje ya uwanja wa muda wa siku saba.

"Nyota wengine wote wako katika hali nzuri na tunatarajia watafanya majukumu yao vyema kama benchi la ufundi litakavyowapa maelekezo," alisema daktari huyo.

Yanga ilianza hatua hiyo ya makundi kwa kupokea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa CR Belouizidad wakati vinara wa Kundi D ni Al Ahly yenye pointi nne ikifuatiwa na Medeama yenye pointi tatu sawa na Waarabu hao wa Algeria.

## Shime afunguka kwenda WAFCON

INATOKA UK. 24

Aliongeza alifanya mabadiliko ya kikosi kutokana na aina ya mchezo waliokuwa wanacheza ugenini, kwa kuamua kupanga wachezaji wenye uwezo wa kukaba na kuzuia mashambulizi kuanzia katikati ya kiwanja na mstari wa mwisho.

"Nawapongeza wachezaji kwa kazi kubwa waliyofanya kuheshimisha taifa kuwa miongoni mwa mataifa 12 yanayokwenda kupeperusha bendera mwakani katika fainali za WAFCON huko Morocco.

Tumejifunza vitu vingi kupitia mchezo huu pamoja na kupoteza lakini tumepata vitu vingi vitakavyotusaidia kuelekea katika mashindano yajayo," alisema kocha huyo.

Naye nahodha wa Twiga Stars, Oppa Clement, alisema haukuwa mchezo rahisi kutokana na ubora wa wapinzani wao lakini walipambana na kufanikiwa kuzuia mashambulizi ingawa walikubali kichapo cha mabao 2-0.

Oppa alisema walipambana kutoruhusu mabao kipindi cha kwanza jambo ambalo walifanikiwa na kufanya waende mapumziko huku kila upande ukiwa haujafunga goli.

"Kipindi cha pili tuliingia na mipango yetu lakini wakafanikiwa kufunga mabao mawili dakika za mwisho, lakini haikuwasaidia, tumefanikiwa kwenda fainali ni jambo la faraja kwetu na linaleta hamasa kuona soka la wanawake Tanzania linapiga hatua," alisema Oppa.

# Michezo

Alhamisi Desemba 7, 2023
Nipashe




**Arteta kuikosa Villa Jumamosi** UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga wakifanya mazoezi kuelekea mechi ya Kundi D ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama itakayochezwa kesho kwenye Mji wa Kumasi, Ghana. **PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI AONGEZA DOZI MPYA YANGA

## ●●● Kocha huyo ajipanga kuonyesha kandanda safi na kiwango bora ili...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanavuna alama tatu muhimu ugenini, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amewaongezea mazoezi wachezaji wake ili kuwajenga zaidi na kuwaweka tayari kuwakabili wapinzani wao Medeama SC kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho mjini Kumasi, Ghana.

Medeama yenye pointi tatu inatarajiwa kuwakaribisha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga katika mchezo wa tatu wa Kundi D huku ikiwa na pointi moja mkononi kutokana na sare ya bao 1-1 waliyopata dhidi ya Al Ahly wiki iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema 'hakuna kulala' baada ya kuwasili katika mji wa Kumasi, kikosi chao kiliendelea na programu ya mazoezi.

Harrison alisema wachezaji walianza na mazoezi ya kupasha misuli na hii ilitokana na kuiweka miili sawa kwa lengo la kuondoa uchovu wa safari.

Alisema programu yao sasa inaonyesha wachezaji watafanya mazoezi mara mbili kwa siku, maandalizi ambayo ni tofauti na michezo iliyopita ambayo walikuwa wakijifua mara moja.

"Jana (juzi) tulifika salama, hatukupata changamoto yoyote, licha ya kuwa na safari ndefu na uchovu wa wachezaji haijatuzuia kuacha mazoezi kwa ajili ya kuwaweka sawa vijana, kesho (leo) tutakuwa na programu ya mazoezi ya uwanjani mara mbili (asubuhi na jioni).

Hali ya hewa ni nzuri, kufika hapa mapema tumelenga kuwafanya wachezaji wazoee hali ya hewa, lakini pia kupata muda wa wachezaji kuzoea mazingira ya uwanja ambao kesho (leo) tutaenda kufanya mazoezi kwenye dimba ambalo tutatumia katika mchezo husika," alisema Harrison.

Aliongeza kocha awao amekuwa makini zaidi na safu ya ulinzi na ushambuliaji ili kuhakikisha mabeki hawaruhusu bao lakini pia washambuliaji wanaongeza utulivu na kutumia nafasi zinazopatikana ili kusaka ushindi.

Alisisitiza malengo yao makubwa ni kutafuta ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kucheza hatua ya robo fainali ya mashindano hayo na wanajua ili kufika huko ni lazima washinde mechi zote

INAENDELEA UK. 23

# Shime afunguka kwenda WAFCON

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kukata tiketi ya kucheza fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024), Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Twiga Stars), Bakari Shime, amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kuipa heshima Tanzania, imeelezwa.

Fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco, zinashirikisha timu 12, Tanzania ikifuzu kwa mara ya tatu.

Licha ya kufungwa mabao 2-0 na wenyeji wao Togo katika mechi ya marudiano ya raundi ya tatu iliyochezwa juzi usiku, Twiga Stars ilifuzu kwa ushindi wa jumla wa magoli 3-2.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime alisema dakika 90 za ugenini zilikuwa na ushindani mkubwa katika mechi hiyo iliyokuwa ngumu kutokana na aina ya wapinzani wao, Togo ambao walijipanga 'kupindua meza'.

Shime alisema baada ya kufahamu mipango ya wenyeji wao, kikosi chake kiliingia uwanjani kwa lengo la kusaka ushindi pamoja na kuzuia wapinzani wao kutofunga mabao zaidi ya matatu.

Kocha huyo alisema walikuwa na nafasi kubwa ya kushinda mechi hiyo hasa kipindi cha kwanza kutokana na nafasi walizotengeneza lakini bahati mbaya washambuliaji walikosa umakini wa kutumia vyema nafasi hizo.

"Kipindi cha pili kilikuwa kigumu zaidi kwa sababu ya wapinzani wetu (Togo) walikuwa wanalazimisha kufika kwa kucheza mpira wa nguvu kwa sababu hawakuwa na chakupoteza, na hiyo iliwasaidia kupata mabao mawili dakika za mwishoni kipindi cha pili.

Niwapongeze wachezaji kukaa vizuri na kuzuia mashambulizi ya hatari, walifanikiwa kuwasukuma katika kona ambayo ni vigumu kwao kupindua meza, lakini walifanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-0 ambayo hayakuwasaidia wao na sisi kufanikiwa kufuzu rasmi," alisema Shime.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >